

BENDERA



Asante, Ndugu Outlaw. Asante sana.

Habari za jioni, rafiki. Hiyo ni ninii... Bila shaka ninathamini utambulisho huo mzuri wa Ndugu Outlaw, na sote wawili tunauhisi. Nami nina furaha kuwa katika maskani hii usiku wa leo, kurudi huku Phoenix, na kusikiliza nyimbo hizi za ajabu na kwaya hii ndogo inayopendeza. Nilikuwa tu nikiwachunguza sana. Ninakosoa sana baadhi ya vile watu wanavyofanya na wanavyovaa nguo katika siku hizi za mwisho, kwa namna fulani ninapendezwa na kundi hili dogo la wanawake wenye nyuso safi hapa juu. Na linaonekana ni jambo zuri sana kwangu. Na hakika ninashukuru sana kwa ajili yao. Mungu awabariki.

² Na kwa Ndugu Outlaw na mwanawe, ninakumbuka wakati nilipokuwa hapa, mvulana huyo alikuwa ni jamaa mdogo tu. Na sasa huyu hapa, nafikiri, ameo na labda ana familia. Na inaonyesha tu hilo halichukui muda mrefu kutukia, sivyo? Hakika tunachukuliwa vivi hivi tu kushuka kwenye hiyo njia. Lakini kuna jambo moja zuri sana tunalotazamia, ile siku tutakayomwona Bwana wetu Yesu, basi ndipo sote tutabadilishwa wakati huo.

³ Walisema Dada Waldrop alikuwa yupo hapa usiku wa leo, yule mama aliyeponywa kansa. Niliita jina lake majuzi usiku. Yuko wapi? Je! yuko hapa jengoni, sasa? Ndiyo, Dada Waldrop, naam, na Ndugu Waldrop pia. Hakika tuna furaha kuwa nanyi ibadani usiku wa leo. Ninaamini ninamwona Ndugu na Dada Evans kutoka Macon, Georgia, hapa upande wa kushoto, kutoka huko mbali Macon kuja hapa.

⁴ Na—na huyu ndugu Mgiriki anayeketi hapa mbele, siwezi kukumbuka. Ametoka huko mbali Ugiriki, kwa hiyo nilikutana naye si muda mrefu uliopita. Na Eddie, ninaamini, sivyo? Ama, mimi ni... [Ndugu huyo anasema, “Dave.”—Mh.] Dave, David. Ninathamini Biblia hiyo, na kadhalika, uliyonitumia hivi majuzi tu, kitabu hicho. Nami ninakushukuru sana, ndugu.

⁵ Na wengi wa marafiki zetu... Lipo kundi lingine kutoka Georgia, Ndugu S. T., ndivyo ninavyomwita, ninaamini, ama T. S., upande *huu*.

⁶ Nami nilifurahi kumwona mvulana wa Ndugu Williams. Ni mara ngapi ambapo ameniomba nimwombee, na kumsikia akisimama hapa na kushuhudia namna hiyo usiku wa leo, hakika liliuchangamsha sana moyo wangu, pia—pia, kwa ajili hiyo.

7 Wakati nikiingia, nilikutana na Ndugu Mc Anally pale nje, rafiki yangu wa zamani. Mimi humwona karibu kila wakati ninaposhuka kuja huku.

Kuna marafiki zetu wengi sana hapa.

8 Nikisikia shuhuda za uponyaji, inaniletea mimi kuwazia jambo hili. Muda mfupi uliopita nilipiga simu ya mbali kwa Ndugu Tommy Hicks, ambaye yuko Washington, ama Oregon, hasa. Alinitaka niende nikachukue mahali pake juma hili. Ndugu yake, na shemeji yake, na familia nzima, waliuawa papo hapo alasiri ya leo, huko Mexico. Naye hana budi kwenda huko kumtambua ndugu yake na kufanya matayarisho yote na kadhalika. Na kwa kweli ninamsikitikia Ndugu Hicks. Ilinibidi kufanya jambo lilo hilo, majuma machache yaliyopita, kwa ajili ya mama yangu. Nami ninajua kabisa jinsi anavyojisikia. Na kwa hiyo, ninaamini, kwenye wakati huu, kwa kuwa tunashirikiana pamoja kama watu wa mwili mmoja mkuu wa Kikristo, ninaamini ingekuwa ni vizuri sana kama tungeinamisha vichwa vyetu kwa dakika moja na kumwombea Ndugu Hicks faraja wakati huu.

9 Baba yetu wa Mbinguni, tunaleta mbele Zako sasa, kama kundi, kundi la watu ambao ni wasafiri na wageni, wapitaji, tukikiri ya kwamba haya si makazi yetu, sisi ni wenyeji wa Ufalme mwingine mkuu ujao, ambao Yesu alitufundisha kuomba, "Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yatimizwe." Baba, usiku wa leo, mmoja wa ndugu zetu, Ndugu Tommy Hicks, mtumishi Wako, huzuni inaelea kupitia kwenye nyaya kuingia masikio yake. Ndugu yake mpenzi, nikiamini alikuwa ni mvulana asiyeokoka, na mkewe, na watoto, wote waliangamizwa leo na ajali ya motokaa. Na ndugu yetu yuko hewani sasa, akisafiri kwenda kuulaki mwili wa ndugu yake wa thamani. Ninamwombea Ndugu Hicks, Bwana. Ninaomba ya kwamba Roho Wako awe juu yake na amsaidie. Mfariji. Na jalia mkono mkuu wa Mungu aliye hai unyooshwe na kumpa neema ya kumshikilia katika wakati huu. Nikihisi hiyo hisi kali kwa nafsi yangu, Bwana, ya majuma machache tu yaliyopita, jambo kama hilo likitukia, nami ninamsikitikia. Nami ninaomba ya kwamba utamfariji kwa kila njia uwezayo, Baba. Tunaomba haya katika Jina la Yesu. Amina.

10 Kuna mambo mengi sana ya kusemwa, wakati ni mdogo sana kuyasema. Tunasikitika sana usiku wa leo, kwamba watu wamesimama humu ndani, nje, na kwenye kuta za kanisa.

11 Sasa, juma hili, Alhamisi ijayo mkutano unaanza juu hapa huko Ramada. Ninaamini nilitamka hilo sawa. Huko upande wa kuume wa Magharibi. . . ama Mtaa wa Mashariki wa VanBuren. Na Ramada, kwa namna fulani ni sebule kubwa pale yenye nafasi ya kutosha ya kuketi watu elfu mbili mia tano. Na imehesabiwa kwamba ni majaliwa makuu kwangu kualikwa

hapa na Ushirika wa Wafanyabiashara wa Full Gospel, ambao nimewahubiria, karibu kote ulimwenguni, kwa ajili yao. Nao walinalika hapa kwenye mkutano huu, Ndugu Williams, na rais hapa wa tawi hili, na wengi wa watu hawa wazuri.

¹² Nasi tunatarajia wakati mkuu kule juu, na kutakuwako na wahubiri wazuri, ninavyofahamu, watakaokuwako huko. Ninasikia ya kwamba yatakuwa ni majaliwa makubwa kwangu kuhubiri kwenye kiamshakinywa cha Jumamosi asubuhi. Na endapo hilo litakuwa hivyo, ninataka kuzungumza juu ya somo: *Mtu Mbaya Sana Niliyepata Kumwona*. Kwa hiyo . . .

¹³ Na halafu Jumapili alasiri napaswa kuhubiri tena, kuuhutubia mwili wa waaminio kule Jumapili alasiri. Kote katika juma hili nina kanisa baada ya kanisa, kanisa baada ya kanisa, mara nyingine mawili katika siku moja, na kwa hiyo, kuwatembelea ndugu zangu. Na kweli ninayahesabu kuwa ni majaliwa, enyi marafiki, kuweza kukutana na madhehebu mbalimbali.

¹⁴ Na hapa, muda mrefu uliopita, jambo hili karibu lingekuwa lisilowezezana, kuwaleta watu pamoja wa makundi mbalimbali na madhehebu. Lakini Mungu ni mwema sana. Ni mwema. Yeye ametenda kazi hivi kwamba wote hao sasa wanaanza kufanya ushirika mmoja na mwingine, na kusahau tofauti zao ndogo ndogo, na kukaza mwendo kuifikia mede ya Wito mkuu. Hilo bila shaka ni jambo zuri. Ninamshukuru sana Mungu, kuona jambo hilo. Na sasa hebu na uendelee kukua, ndilo ombi langu.

¹⁵ Ndugu Outlaw, kama vile alivyosema sasa hivi, alikuwa wa kwanza kunialika Phoenix. Nilikuja hapa miaka mingi iliyopita pamoja na Ndugu Kidson, nasi tulikuwa na mkutano mkuu. Mkutano huo ulikuwa ni tukio kuu sana katika maisha yangu. Hawakuwa na vinasasauti wakati huo. Walikuwa na kinakili sauti kidogo nao walitengeneza santuri. Nami ningali nina santuri zilizotengenezwa kutoka kwenye kanisa la Ndugu Outlaw, na kutoka kwenye kanisa la Ndugu Garcia huko, maskini ile kwaya ya Kihispaniola iliyoimba katika Kihispaniola, kama hawa wanavyofanya katika—katika Kiingereza.

¹⁶ Na mara kwa mara kwa namna fulani tunakuwa wapweke nyumbani, nami kwa namna fulani ninapata huzuni, kuwaona hawa jamaa, unaona, jamaa wanaotoka Phoenix. Ninaweka rekodi hiyo na kuicheza, mwajua. Nanyi. . . Karibu imechakaa kabisa. Lakini ninajua vizuri sana, hata ninajua kila wakati mdogo itakaporuka na kuruka mstari, na kadhalika, kwa hiyo ninadumu tu moja kwa moja nayo.

¹⁷ Nimekuwa na tukio la kuhuzunisha sana maishani mwangu hivi majuzi, la kumpoteza mama yangu, ambaye alikuwa ni Mkristo mzuri sana. Lakini kuondoka kwa—kwake kulikuwa kwa haraka. Sina wakati wa kusimulia jambo hilo usiku wa leo.

Ninataka kuninii, katika mmoja wa mikutano, siku fulani ya viamshakinywa vidogo mahali fulani, na jinsi ambavyo Bwana alinituma niende zangu, jambo hili lipate kutukia. Alinipa ono kunionyesha mahali pa kwenda na kile kingetukia. Ndipo, nilipokuwa nikirudi. . . Na utamu wa kumwangualia mama akifikia mwisho wa safari yake, nikimshika mikononi mwangu, ama kumshika mkono, na kuikabidhi nafsi yake kwa Mungu, na kumwona maskini kipenzi huyo mwanamke mzee, mtakatifu, alipokuwa akitoka, wakati asingeweza kuzungumza tena.

¹⁸ Nami nikasema, “Mama, je! Yesu angali ni mtamu sana kwako kama alivyokuwa ile siku ulipompokea Roho Mtakatifu? Huwezi kuzungumza, ninajua. Lakini kama ni halisi, pepesa tu macho yako haraka sana.” Naye angepepesa macho yake, na machozi yangetiririka tu mashavuni mwake. Naye akaenda kukutana na Bwana. Usiku huo Yeye alinjia katika ono na akanionyesha mama, jinsi alivyokuwa wakati huo. Siwezi kuacha kuwaalika watu wajitahidi sana kwenda Huko. Unaona? Kuweka. . . Kamwe usikose jambo hilo, ewe rafiki.

¹⁹ Na sasa, mara nyingi, jinsi tunavyosimama, hatumfukuzi mtu yeyote kwenye ushirika kwa ajili ya vile wanavyoamini, lakini kwa kuwa sisi ni wapentekoste, na tukiwa na ujuzi wa kipentekoste, nimeona jambo hilo likija kwenye familia yangu, wale waliofikia moja kwa moja kwenye mwisho wa safari, na kuwaangualia mpaka nafsi yao ilipotoka. Ninawaambia, nina furaha sana kwamba nina tukio la hilo. Mimi. . . ya kuwa ni ujuzi wa kipentekoste ndani yangu. Nami ninataka tu kila mtu awe nalo. Msilikose. Lolote mfanyalo, msilikose tukio hilo.

²⁰ Kwa kawaida katika mikutano yangu, kila mahali niendapo, daima inahusu kuwaombea wagonjwa. Sijui. I—imekuwa na ufanisi mkuu sana. Bwana amebariki, akiyajibu maombi yangu mara nyingi. Nami nauliza, kabla tu sijawahutubia, je! kuna mtu aliyekuja usiku wa leo akaombewe, jambo fulani, kusudi nibadilisha somo langu kidogo. Mlikuwa mwombewe, nilikuwa nikitaka kuzungumza jambo fulani juu ya uponyaji wa Kiungu. Kama hakuna, nilikuwa nikitaka kuzungumzia jambo lingine. Je! kuna mtu hapa wa kuombewa, angetaka kuombewa? Inua mkono wako, kusudi nipate dokezo. A-ha. Jamani! Vema, nilimenyana karibu nusu saa, muda mfupi uliopita.

²¹ Hebu, jambo lingine, je! Billy Paul yupo hapa, mwanangu? Billy Paul, je! upo hapa? Una kadi za maombi huko nje? Nenda ukachukue baadhi, wakati nikizungumza kidogo, uzisambaze. Unaona?

²² Kama hufanyi hivyo, mara nyingi wanaendelea kurudi na kurudi, na huku na huko, mstarini namna hiyo. Kamwe hufikii mwisho wake. Naam. Kwa hiyo u. . . Na kwa hiyo, kama utakuwa na idadi hiyo, tunataka kila mmoja wao, lakini si mara mbili, unaona. Hatuwezi. Maana, wengi wa watu hapa wametoka

mbali. Nami nitazungumza kimyakimya kwa muda mfupi tu juu ya jambo moja ama lingine ambalo litajaribu kusaidia, na kuleta imani kwenye kiwango kile ambapo tunaweza kuwaombea wagonjwa.

²³ Mna mchungaji mzuri sana, na mchungaji mwenza hapa, halmashauri nzuri sana, kanisa zuri sana, watu wazuri sana.

²⁴ Na hivi majuzi nilikuwa nikizungumza kwenye mmoja wa mikutano hapa nje Phoenix, katika mkutano wa kwanza. Nilikuwa nikisema, wakati mimi na mke wangu tulipokuwa tukishuka barabarani, mbona, jinsi ambavyo bonde hili lilionekana miaka mia kadhaa iliyopita, na jinsi linavyoonekana siku hizi.

²⁵ Na leo tulisafiri na tukapanda Mlima wa Kusini, na kwenda huko juu kabisa juu ya ule mji pale, nje ya mazingira ya mji. Tulikuwa tumeketi pamoja kule tukizungumza juu ya Bwana, na jinsi ambavyo amekuwa mwema kwetu. Na ninii tu... Roho Mtakatifu kwa utamu sana akaingia ndani ya gari. Na ninii tu. . .

²⁶ Ndipo nikaangalia chini kwenye bonde ambapo mimi na mtoto Joseph tulishuka, si muda mrefu uliopita, wakati nilipokuwa hapa. Na mimi na yeye tuliketi kule chini, tukashikana mikono, na kuomba, mvulana wangu mdogo. Ndipo nikamwomba Mungu, nitakapoondoka, anijalie niweze kuiweka Biblia yangu mikononi mwake, na amjalie adumu nayo, na Neno tu, nao utakuwa ni mchango wangu Kwake kwa kuyahifadhi maisha yangu na kunisaidia.

²⁷ Sasa, mnajua, kama mkiondoka! Tunajua, miji yote. Nafikiri Phoenix ni—ni mji unaopendeza.

²⁸ Lakini nilimwambia mke wangu, “Hebu wazia tu, kule chini sasa, wakati uu huu, bonde lile dogo, Bonde la Maricopa hapa, tunavyoweza kuliangalia, Mto wa Chumvi, unaopitia hapa, ni watu wangapi wakati huu, katika bonde hilo moja dogo, wanaapa bure kwa Jina la Bwana! Ni dhambi ngapi, uzinzi, na kadhalika, zimefanywa katika saa moja iliyopita, katika mji huu, kundi hili dogo la watu!” Nikasema, “Unafikiri ni watu wangapi wamefanya dhambi katika dakika kumi na tano zilizopita, tangu tulipokuwa tumeketi hapa katika mji huu?” Wazia jambo hilo, usiku wa leo. Nikasema, “Ni ajabu ya kwamba Mungu hakifagilii mbali kitu hicho, namna hiyo.” Bila shaka ni kweli.

²⁹ Lakini je! mnakumbuka kama ilivyokuwa katika Sodoma? Kulikuwako na mtu fulani kule chini aliyekuwa atolewe. Nami nikasema, “Mpenzi, mbali na hayo yote, kumbuka, kwamba katika bonde hili tangu tumekuwa hapa juu, kumekuwako na ombi baada ya ombi lililotoka kwenye moyo mwaminifu. Unaona?” Kisha nikasema, “Hiyo ndiyo sababu tuko hapa Phoenix leo, na katika mikutano hii hapa, ule ushirika pamoja

na ndugu zetu, ni kujiweka pamoja nao, kusaidia kusukuma mzigo huu mkubwa, kujaribu kuwafanya wengine waone.”

³⁰ Sasa, siku moja ninaamini ya kwamba bonde lote zima litafagiliwa mbali. Ulimwengu wote utafagiliwa mbali, na ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu utakuja.” Ndipo nikasema, “Askari wa vita na mashujaa wa imani basi watatembea kwenye bustani za Mungu, hawatazeeka tena, hawatakuwa wagonjwa tena, wakati nyimbo za furaha zikijaa hewani, Malaika wakiangalia chini.”

³¹ Ninawazia juu ya askari akirudi nyumbani wakati akisifiwa kwa heshima, unajua, nchi za ng’ambo ama chochote kile, na jinsi ambavyo inaonekana kwamba kuna heshima kuu anayopewa na watu. Lakini ni kitu gani? Ni heshima chache tu huko mitaani, na sauti chache za baragumu kutolewa, ama kengele kupigwa, halafu unarejea kwenye ile hali ya zamani.

³² Lakini upande huu mwingine hii itakuwa ni Umilele usio na mwisho, jinsi ambavyo nyi—nyimbo za furaha za Malaika wakiimba, wakati mashujaa hawa na wake zao na familia wakipita kwenye furaha kuu za Mungu. Sasa, hizo si ndoto fulani za kisasili kama za Baba Krismasi. Hiyo ni kweli, enyi marafiki. Na—na tunatarajia jambo hilo. Ninatazamia, kwa moyo wangu wote, kwenye wakati Kristo atakapokuja nasi tutakuwa katika mfano Wake wakati huo, na hakutakuwako na uzee tena.

Wasemaje? Njoo papa hapa, Paul, tafadhali.

³³ Nanyi mnaotaka kadi ya maombi, wakati akija huku, kuwapa tu kadi ya maombi, inueni tu mikono yenu.

³⁴ Nami sijui kama ingekuwa ni kuuliza mengi mno, kama tungewapata mpiga piano huyu na kwaya hii kuimba?

³⁵ Vema, hebu na tuwe na wasikilizaji, tumshirikishe kila mtu, wakipenda, waimbe *Karibu Na Wewe. Karibu Na Wewe*. Mnajua wimbo huo? Mnaujua? Kila mtu anaujua? *Karibu Na Wewe?* Vema.

³⁶ Wimbo fulani, hebu tuiache kwaya iimbe mmoja basi. Hilo, nafikiri hilo lingekuwa ni jema zaidi, afadhali tuiache kwaya iimbe. Hilo litawafanya nyote mpende kutoa, kuchukua kadi zenu za maombi.

³⁷ Ndugu Outlaw, waweza kuja hapa tena, tafadhali, kama sio kukuomba mengi mno, ndugu yangu? Nasi tutaimba pambio lingine, ama chochote kile, kutoka kwa watu. Na kisha tutaenda moja kwa moja, upesi tuwezavyo, kwenye Ujumbe mfupi, na kuwaombea wagonjwa. Bwana awabariki. Ombeeni kwaya hii ndogo sasa, wakati ikininii...wote wanaowathamini. Ninyi wapentekoste mnaothamini kundi dogo zuri, la wasichana na wavulana linaloonekana safi jinsi hiyo, inueni tu mikono yenu. Mnaona? Hakika tunalithamini. Kuna jambo moja zuri sana,

mambo mengi mazuri sana, kuhusu kanisa hili hapa, na, moja ya hayo, hakika wao ni waimbaji kweli.

³⁸ [Ndugu Billy Paul Branham anasambaza kadi za maombi, kwa kama dakika saba, wakati kwaya ikiimba *Yesu Ni Rafiki Yangu*, ama, *Yesu Atanifanikisha*. Kiongozi wa kwaya ndipo anasema, “Billy alisema tuimbe ‘*Kuondoka...?...*’ Lakini tunataka kuimba wimbo tulioimba hivi majuzi usiku. Tusingeonekana kufanikiwa, vivyo hivyo na Jumanne usiku, mpaka tulipouimba wimbo huu, kwa hiyo tutajaribu kuuimba sasa. *Nilikuwapo Wakati Roho Alipokuja*. Ni wangapi walio na Roho?” Kusanyiko linasema, “Amina.” Kiongozi wa kwaya anasema, “Ni wangapi walio na Roho Mtakatifu?” Kusanyiko linasema, “Amina.” Kiongozi wa kwaya anasema, “Kwa hiyo, *Nilikuwapo Wakati Roho Alipokuja*.” Kwaya sasa inaimba *Nilikuwapo Wakati Roho Alipokuja*—Mh.]

³⁹ Bwana ashukuriwe kwa hilo. Amina. Jinsi tulivyo na shukrani kwa ajili ya kuhuishwa kuzuri kwa kiroho namna hiyo! *Nilikuwapo Wakati Roho Alipokuja*.

⁴⁰ Sasa, tunashukuru kwa ajili ya ibada hizi, tena ninasema, nasi tunaomba sasa ya kwamba Mungu atawaponya wagonjwa, atawaokoa waliopotea.

⁴¹ Sasa, niombeeni. Sasa, mnapoingia, kwa namna fulani bila kutarajiwa, nasi hatujui matayarisho yoyote; kuingia tu na kutoka, na namna hiyo, hatuwezi kujisikia kana kwamba hatufanyi vizuri tuwezavyo kwa ajili ya Bwana, bali tunajaribu kufanya vizuri tuwezavyo kwa ajili Yake.

Kwa hiyo hebu na tuinamishe vichwa vyetu mara nyingine tena kwa ajili ya maombi.

⁴² Baba yetu wa Mbinguni, ni usiku wa leo, tukiwa na mioyo yenye shukrani, ambapo tunakabili kiti Chako cha enzi, bila kujua kwamba mapenzi Yako ni yapi, na kile kitupasacho kufanya. Lakini Wewe utatungoza. Uliahidi kutungoza, kwa hiyo tunaamini jambo hilo. Tunaomba ya kwamba utasema na waliopotea usiku wa leo, na utawaponya wagonjwa. Utajipatia Utukufu.

⁴³ Bariki kanisa hili, tunaomba tena, Bwana. Bariki kila kanisa lililo katika mji huu na katika bonde hili, kwamba wakati utakuja ambapo kutakuwa na umwagikaji mkuu wa Roho juu ya watu hawa wote, ili kwamba watu kutoka kila mahali nchini watajaa humu kwa wingi kulisikia Neno la Bwana.

⁴⁴ Sasa, tunatambua, Bwana, sababu ambayo tunaweza kufurahi na kuimba nyimbo ni, kwanza, kwa sababu tulikuja kwa Kristo, tukiamini ya kwamba Yeye alikuwa ndiye. “Kwa kuwa imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno.” Na kwa vile tumefurahia kuimba nyimbo za kiroho, na kuona Roho akitenda kazi katika wasikilizaji, sasa naomba utoe Neno ambalo litaitayarisha mioyo ya watu kwa ajili ya ibada ijayo, kwa ajili

ya kuponywa kwa wagonjwa, na kuponywa kiroho kwa mtu aliyejeruhiwa, ama maskini dhamira changa iliyochubuliwa, kama mwanzi uliopondeka. Tunaomba ya kwamba utaitia nguvu usiku wa leo, Bwana, na kuipa zeri Yako inayoponya ambayo itatoa tiba kwa ajili ya wote, kusudi huyo mmoja ambaye huenda aliondolewa Njiani atarejeshwa Njiani usiku wa leo.

⁴⁵ Pia tungeomba, Bwana, kwa ajili ya wale walioko hospitalini, wagonjwa sana hata hawawezi kuenda ibadani. Tunawaomba, tukijua ya kwamba wangependa kuwa hapa, bali adui amewafunga hivi kwamba wasingeweza kuja. Mungu, jalia ya kwamba ukombozi wao uje upesi. Tunaamini ya kwamba imeandikwa katika Neno, ya kwamba, “Watu wanaoitwa kwa Jina Langu watakusanyika pamoja na kuomba, ndipo nitasikia kutoka Mbinguni.” Hiyo ndiyo sababu tunachukua nafasi hii kuomba wakati makanisa yote yanapokusanyika pamoja, ili kwamba Wewe usikie kutoka Mbinguni na kuiponya nchi yetu. Tunaomba jambo hili sasa kwa ajili ya utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

⁴⁶ Sasa, ninawasikitikia wale wanaosimama, na miguu ikichoka, nitaharakisha upesi tu niwezavyo. Ningetaka kurudi wakati mwingine huku Phoenix, na ambapo tungemleta kila mtu pamoja, tuwe na ibada nzuri, ndefu, ya uponyaji katika Phoenix, ambapo Bwana atabariki baadhi yetu. Baadhi yetu ni wahubiri, kama vile Ndugu Outlaw. Na wengi wa hao ndugu wengine hapa ni wahubiri. Mimi si mhubiri sana. Ni—ninawaomba tu wagonjwa. Na hata hivyo hakuna mtu aliyewahi kuihubiri Injili bila kupenda kuwaelezea watu jinsi anavyojisikia. Kuna kitu fulani tu kuhusu jambo hilo, unapenda kufanya jambo hilo. Nami nina furaha sana ya kwamba mmekuja ku—kusikia maelezo madogo niliyo nayo kumhusu Yeye, na natumaini ya kwamba Yeye atafanya jambo fulani usiku wa leo kuwathibitishia ya kwamba ni—ninawaambia Ukweli na ninawapenda.

⁴⁷ Ninataka kuchukua fungu dogo hapa kwa dakika chache, Bwana akipenda, kutoka katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 12 na kifungu cha 32.

Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu.

⁴⁸ Na kwa ajili ya somo dogo, kujenga juu ya hilo, ningetaka kuchukua somo la: *Bendera*.

⁴⁹ Hilo ni jambo la kipekee sana, la ajabu, kusoma fungu kama hilo, ama kusoma Andiko, halafu kuchukua somo la kipekee. Lakini nimekuta katika miaka ya huduma, ya kwamba wakati mwingine Mungu huja kwa njia ya kipekee, nyakati za kipekee, nyakati ambapo huwazii, ananena kupitia mafungu ambayo tusingewazia kwamba angezungumza kupitia hayo, anatomia

mtu ambaye tungewazia angekuwa duni. Lakini Mungu hutenda kazi katika njia za kisiri, kutenda maajabu Yake.

⁵⁰ Na bendera, hakika, sote tunajua bendera ni kitu gani. Ni kitu ambacho ni kumbukumbu, kitu fulani kilichoinuliwa, kwa watu, cha kuangaliwa. Ni kitu fulani kilichowekwa mbele zako. Na Mungu aliahidi, katika Isaya, mlango wa 5 na kifungu cha 26, ya kwamba, “Kungekuwako na bendera itakayoinuliwa. Kungekuwako na bendera itakayoinuliwa.”

⁵¹ Mwanadamu kote katika nyakati anaelekea, liko ndani yake, kujaribu kujisaidia mwenyewe. Sasa, hiyo ni tabia tu ya mwanadamu.

⁵² Sasa, kile tunachojaribu kufanya ni kuweka msingi hapa kwa ajili ya jambo fulani tunalomwomba Bwana kufanya: kuwaponya wagonjwa, na kututia moyo. Nawe huwezi tu kutoka moja kwa moja uende na kuwa na imani kwa kitu ambacho hujui kitu kukihusu. Inakubidi kwanza kuwa na kitu ambacho imani itatulia juu yake.

⁵³ Ulipomwoa mke wako, ilikubidi uwe na imani naye. Ilimbidi yeye awe na imani nawe, kabla hamjaweza kuwa familia. Wala huwezi kuokota kitu vivi hivi na uwe na imani nacho, kwa sababu hakijathibitishwa.

⁵⁴ Kwa hiyo kitu kilichothibitishwa sana ambacho tungeweka msingi juu yake, kwa imani, kingekuwa ni Neno la Mungu. “Kwa maana imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia Neno la Mungu,” kwa sababu ni Neno la Mungu.

⁵⁵ Na mwanadamu sasa, kwa kuwa ameumbwa, hata katika hali yake ya kuanguka, hata hivyo yeye yuko katika umbo la Muumba Wake, Mungu. Na katika maana moja ya neno, yeye ni mwana wa Mungu, aliyeanguka kutoka kwenye neema. Ameanguka kutoka kwenye kitu kile Mungu alichomfanya kuwa. Na katika hali yake ya kuanguka, inampa sifa za kujaribu kufanya jambo fulani apate kujirudisha kwenye mahali ambapo kitu fulani ndani yake kinamwambia ya kwamba alitoka hapo. Kwa sababu, yeye anajua hayuko katika hali halisi bado, maana anaona mauti, maradhi, na huzuni, na huzuni ya moyoni, na maudhi. Yeye anajua hakuumbwa kwa ajili ya jambo hilo. Hata hivyo, haidhuru yeye yuko umbali gani na Mungu, kuna kitu fulani ndani yake kinachomwambia hivyo, kitu fulani humo ndani.

Sasa, mtu ameumbwa kiumbe chenye asili tatu: nafsi, mwili, roho.

⁵⁶ Sasa, nje ni mwili. Kuna milango mitano ya kuingia kwenye mwili huo, na naam hiyo ni zile hisi tano, hakika: kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia.

⁵⁷ Mle ndani, kama mbegu iliyopandwa, ndani yake ni kitu chororo cha mbegu, ambacho ni nafsi. Kuna milango mitano

ya kuingia humo, unayoingilia: dhamira, na kumbukumbu, na kadhalika.

⁵⁸ Lakini basi ndani ya chumba hicho kidogo kuna chumba cha tatu, ambacho ni roho. Na hiyo ndiyo inayoongoza hizo zingine. Kuna njia moja tu ya kuingia humo, na hiyo ni hiari ya mtu. Unaweza kuikubali ama kuikataa, na hiyo ndiyo njia pekee ya kuingia humo. Kama ukiyakubali mapenzi ya Mungu kupitia roho huyo, Roho wa Mungu anachukua nafasi Yake ndani ya moyo wako na kukutawala wewe mzima. Na usipokubali jambo Hilo, basi adui anashika hatamu na kukutawala wewe mzima. Kwa hiyo inategemea jambo hilo.

⁵⁹ Na mwanadamu, kwa kuwa ameumbwa jinsi hiyo, basi inampa ki—kitu fulani ndani yake kinachomfanya atake kufanikisha jambo fulani kwa nafsi yake. Anajaribu kufanya kitu fulani kujiokoa. Anataka kutoka ndani ya kitu hicho, lakini anataka kufanya hivyo yeye mwenyewe. Anataka kujifanyia njia yake mwenyewe kwa jambo hilo.

⁶⁰ Sasa, amejaribu ufanisi mwingi. Amejaribu kufanikisha hili kupitia sayansi. Na kila wakati anapopitia kwa sayansi, anajiangamiza tu mwenyewe. Kila wakati sayansi inapobuni kitu, yeye hujiangamiza mwenyewe; baruti, na nguvu za atomiki, na—na zana za nyuklia, na magari, na vitu hivi vyote. Hata hivyo, inamsaidia kwa muda, lakini hatimaye inamwangamiza. Kwa sababu yeye ni . . . Ni jambo ambalo amefanikisha wakati akiwa katika karakana ya Mungu, akijaribu kuunda kitu, kupotosha kile ambacho Mungu amefanya, na kukiweka katika mawazo yake mwenyewe, na kukibuni.

⁶¹ Sasa, kama nilivyosema juu ya mji huu, kama mji huu mkuu mzuri hapa. Kama mji huu ungalikuwa ninii tu . . . Ungekuwa mzuri kuliko ulivyokuwa mara ya kwanza kama, huku na huko mitaani walitembea watu wa Mungu, huku wameinua mikono yao juu hewani, wakimsifu Mungu kwa ajili ya makazi yao na kila kitu. Hivi Phoenix isingekuwa bustani halisi ya dunia? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Lakini, badala yake, kama miji mingine yote, unadanganya, unaiba, unahadaa, unacheza karata, unavuta sigara, unakunywa pombe, unafanya karamu za ulevi, una uzinzi. Na umekuwa uvundo mbele za Mungu. Mnaona?

⁶² Kwa hiyo, mnaona, kile binadamu anachojaribu kufanikisha, anavuruga yote tu. Hawezi kujiokoa. Naye anapojaribu kwa elimu, ameendea njia hiyo, kuona kama asingeweza kuwaelimisha watu wayafikie maarifa ya wokovu wa Kristo, ama maarifa ya wokovu wake mwenyewe, ama kufanya kitu fulani kupitia kwa elimu yake.

⁶³ Nilikuwa nikisoma hivi majuzi katika—katika gazeti la *Life*. Ambapo, walikuwa na . . . Ninaamini wengi wenu mlisoma makala hiyo. Ambapo, wamefanya kila kitu sasa katika

kuunganisha elementi mbalimbali, ama kuzikusanya, hata karibu wangeweza kuumba uhai. Nao walisema watauumba. Hawataweza kufanya jambo hilo. Uhai ni uumbaji. Kwa hiyo ni mmoja tu aliye Muumba, na huyo ni Mungu. Mnaona? Kamwe hawataweza kufanya uhai, bali yeye anajaribu kufanya hivyo. Nashangaa ingekuwa spishi ya aina gani, kama angaliweza kuiumba, kama ingetokana na akili ya mwanadamu? Kwa hiyo unaona hawezi kufanya hivyo. Hiyo kamwe haiko kwake kufanya hivyo. Ameshindwa kwa elimu. Ameshindwa kwa sayansi.

⁶⁴ Yeye anajua ya kwamba alitoka mahali fulani, bali anataka kutafuta njia ya kurudi.

⁶⁵ Adamu kweli alionyesha jambo hilo, mtu wa kwanza duniani. Baada ya kukuta kwamba alikuwa ameanguka kutoka kwenye neema, yeye alijaribu kuchukua akili yake mwenyewe na kufanya njia ya kurudi kwa Mungu bila ya upatanisho. Alijaribu kurudi kwa Mungu bila kufanya u—upatanisho, kitu fulani cha kulipia dhambi zake. Baada ya adhabu ya Mungu kuwa ni mauti, yeye alijaribu kurudi bila upatanisho wa mauti.

⁶⁶ Na wanadamu wangali wanajaribu kufanya jambo hilo, kujaribu kuunda dini isiyokuwa na upatanisho. Adamu alijitengezea kifuniko kutokana na majani ya mtini, bila ya kumwagwa kwa damu kwa ajili ya kifuniko hiki, na Mungu akayakataa. Na ameyakataa wakati huo, na atayakataa daima. Kwa sababu, “Bila kumwagwa kwa damu hakuna ondoleo la dhambi.”

⁶⁷ Kamwe hawezi kurudi. Kwa sababu, adhabu ni mauti; na kitu fulani hakina budi kufa, kulipia adhabu hiyo. Kwa hiyo kinaweza tu kuwa ni kabadala, vinginevyo sisi sote tuko katika mauti kama kusingekuwako na kabadala chetu cha kushikilia. Naye mwanadamu, katika kufanya jambo hili, alitambua ya kwamba, ya kwamba anahitaji kitu cha kushikilia, kitu ambacho anaweza kuweka mikono yake juu yake, kitu fulani anachoweza kusema, “Hiki ndicho. Nimekipata. Ninajua ndicho.”

⁶⁸ Kwa hiyo, Adamu, ili kushikilia kitu fulani, alifanya jani la mtini apate kuufunika uchi wake na wa mkewe, bali alikuta kwamba kile alichokuwa nacho mkononi mwake hakikufanya kazi.

⁶⁹ Kote katika nyakati zilizopita tungeweza kuwahesabu watu, kama tu tungalikuwa na wakati. Hebu tuchukue wawili ama watatu wao, kwa vyovyote vile.

⁷⁰ Hebu tumchukue Nimrodi. Nimrodi aliwazia jambo lile lile. Baada ya ile gharika, alijua ya kwamba kulikuwako na Mungu Ambaye angewahukumu waovu, kwa kuwa walikuwa tu ndio kwanza watoke kwenye ile gharika. Naye alijua ya kwamba dhambi ndiyo iliyomfanya Mungu kuuangamiza ulimwengu. Kwa hiyo, akijua ya kwamba dhambi tena ingemfanya Mungu

afanye jambo lile lile, yeye alijaribu kufanikisha jambo fulani, kujenga mnara. Ili kwamba, watu wangeweza kukimbia waingie mbinguni kama mambo yakiharibika hapa duniani, na waishi mbinguni; kisha warudi tena duniani, na kutenda dhambi, kisha warudi mbinguni tena.

⁷¹ Sasa, hilo limekuwa ndilo wazo la wanadamu kote katika safari, kujaribu kutenda dhambi na kuishi duniani, na kuwa Mbinguni wakati ule ule. Huwezi kufanya jambo hilo. Huwezi kufanya jambo hilo. Yesu alisema, “Huwezi kumtumikia Mungu na mali.”

⁷² Hiyo ndiyo sababu tunaamini usiku wa leo katika kuachana na dhambi kabisa, kuiondokea. Ni sumu. Usijipumbaze karibu nayo. Usiivumilie hata kidogo. Usiwe na uhusiano wowote nayo. Usione jinsi unavyoweza kuikaribia bila kutenda dhambi. Angalia jinsi unavyoweza kukaa mbali nayo. Kitu chochote kinachoonekana ni dhambi, kaa mbali nacho. Usiwe na uhusiano wowote nacho, hata kidogo.

⁷³ Kwa hiyo, Nimrodi, akiwa na utaalumu wake mwingi, alijaribu kufanikisha jambo hili. Na kama utaangalia, daima imekuwa, tangu mwanadamu alipoumbwa. Kwamba ninii. . . Kama ukifuatilia ukoo wa watoto wa Kaini, wote wanakuwa wanasayansi, watu wenye nguvu, wafanya kazi wa chuma na mbao duniani, na kadhalika. Walikuwa ni wa upande wenye werevu, wenye akili.

Bali watoto wa Sethi walikuwa wakulima wadogo, wachunga kondoo, wanyenyekevu.

⁷⁴ Sasa, hivyo ndivyo ilivyo leo. Hao wanaotegemea kitu fulani cha kimitambo kilichobuniwa na mwanadamu wanachoweza kukishika, waseme, “Hiki ndicho. Hiki ndicho,” kitu ambacho mwanadamu amefanikisha, mwenyewe. Ndipo unaona, sana sana, hao ndio aina ya wanaojaribu kuepukana na upatanisho wa Damu kurudi kwenye Njia ya kweli.

⁷⁵ Sasa, lakini Nimrodi baada ya kitambo kidogo katika kujenga mnara wake, Mungu aliketi mbinguni na kumcheka. Naye akafikia karibu kumalizia. Nataka mwone kwamba yeye alikuwa karibu kufanikisha kile alichooanza kufanya. Lakini, basi, kwa ghafla, Mungu aligeuza kitu hicho vinginevyo, na kitu hicho kikapomoka. Kikawa ni mavumbi. Kama tu vile aproni ya jani la mtini ya Adamu ilivyoangamia, ndivyo mnara wa Nimrodi ulivyoangamia.

⁷⁶ Ndipo akaja mwingine, ambaye alikuwa ni Mfalme Nebukadreza, naye alikuwa akitaka kujenga mji.

⁷⁷ Na kama utaangalia, mara nyingine roho hao ambao huwaingia watu. Na ipo siku inayokuja, na sasa imewadia, ambapo Kanisa la Kikristo, Kanisa la Bwana Yesu Kristo, linapaswa kuwa ni la kiroho sana, kwa kuwa Yesu alisema, ya kwamba, “Roho hao wawili wangepanana sana hata

ingewadangnya walio Wateule kama yamkini.” Adui ni mjanja sana.

⁷⁸ Sasa mwangalie kwa Nebukadreza. Alijenga mji uliofanana sana na Mbinguni, kwa kuwa mto Frati ulipitia—ulipitia kwenye kiti cha enzi. Kama vile Mbinguni, mto wa maji ya Uzima unapitia kwenye Kiti cha Enzi, bustani zinazobembea na kila kitu kama tu vile ilivyokuwa, hapo awali, hata, wakati Ibrahimu alipokuwa akisafiri, akiutafuta Mji kama huo. Na kama wewe si wa kiroho, Shetani atakupofusha kwenye mambo haya, unaona, kitu kinachoonekana kinafanana sana Nacho, bali Sicho. Kama ni cha kujibunia, hakifai kitu. Kama kimenunuliwa kwa Damu na Mungu, ni cha Kweli. Hiyo, mnaona, ni kweli. Lakini, kama ni cha kujibunia. . .

⁷⁹ Sasa, yeye alijenga mji huu mkubwa. Na halafu tunaona ya kwamba, pia, aliwafanyia watu sanamu wapate kuiabudu, na akaleta ibada ya sanamu miongoni mwa watu. Lakini katikati ya hayo yote, kulitokea maandiko ya mkono ya kimbinguni kwenye ukuta, lugha isiyojulikana ambayo hakuna mtu angaliweza kufasiri ila nabii aliyejazwa na Roho aliyekuwa kati yao. Na ufalme huo ukaangamia kwenda mavumbini, kama tu vile mnara wa Nimrodi na aproni ya Adamu ya mtini, vivyo hivyo hasa, kwa sababu ni kitu ambacho mwanadamu alifanikisha mwenyewe. Ni kitu ambacho alitaka kufanya, kuonyesha ya kwamba angeweza kujiokoa.

⁸⁰ Huwezi kujiokoa. Hakuna kitu unachoweza kufanya juu ya jambo hilo. Njia tayari imeandaliwa kwa ajili yako. Huwezi kujiokoa.

⁸¹ Tungeweza kutaja mambo mengine mengi makubwa yaliyotukia. Hivi juzi juzi tu, Ufaransa, baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia walitaka kujenga mahali pale ngome ya Siegfried. Nao wakaelekeza bunduki zao zote kuelekea Ujerumani na kusema, “Sasa, kama Wajerumani wakati wowote wakijaribu kuja huku tena, mbona, tutaweza kuwazuia, kwa maana tuna ngome hapa tunayoweza kuwazuia kwayo.” Kuonyesha tu ya kwamba maazimio ya kujibunia hayawezi kusimama, Wajerumani waliwashinda kwa akili. Walienda nyuma ya ngome hiyo ya Siegfried na kusema, “Tunaweza kula, kunywa, na kuishi katika uzinzi, kucheza dansi, kuishi katika dhambi, kufanya lolote tunalotaka, kwa sababu tumelindwa. Tumefanya kitu ambacho kitatulinda.”

⁸² Wajerumani walienda taratibu moja kwa moja nyuma ya ngome hiyo na kuwateka, mnaona, waliwazunguka moja kwa moja. Kwa sababu, walisahau kuzifanya bunduki zao kuwa zenye mizinga, kuweza kugeuka upande wowote. Kwa hiyo Wajerumani waliondoka tu kwenye upeo wa bunduki zao, na wakazunguka moja kwa moja, nyuma yao, ndipo ngome ya Siegfried ikaanguka.

⁸³ Wajerumani walijitokeza na kujenga ngome ya Maginot. Nao wakawazia, “Kama Wamarekani wakija hapa wakati wowote, mbona, tutaingia katika zege hili imara, nasi tutakuwa sawa.” Ni kitu gani kilichotukia? Wamarekani walikuja kule wakiwa na vifaruu vya makombora na kuwalipua vipandevipande. Ilianguka hata hivyo.

⁸⁴ Marekani, hapa si muda mrefu uliopita, walidhani wangeweza kujenga meli ambayo hakuna wajenzi wengine wa meli wangeweza kujenga. Iliitwa Titanic. Usiku mmoja, wakati ilipokuwa ikitimua mbio baharini huku mitambo yake yote ikifanya kazi, na bendi zilikuwa zikicheza muziki wa jazi, wakifanya shamrashamra. Kwa ghafla, hali iligeuka ikawa *Karibu Na Weve, Mungu Wangu*. Kwa sababu gani? Iligonga genge la barafu huko nje, na kutoboa shimo ndani yake, na kuilipua mitambo, nayo ikazama chini ya bahari. Kwa nini? Mungu kwa mkono Wake wenye nguvu huonyesha ulimwengu huu hauwezi kusimama. Mwanadamu hawezi kufanikisha chochote kwa nafsi yake.

⁸⁵ Sasa, leo, kizaazaa kikubwa kinaendelea, kuhusu zana na nyuklia. Nasi tunatumia mabilioni ya dola kujaribu kumpeleka mtu mwezini. Itafaa nini baada ya yeye kufika mwezini? Mimi sininii. . . Kama nilivyosema hivi majuzi usiku, sihofu juu ya kufika mwezini. Ninataka kufika Mbinguni, kwa hiyo kwangu mimi mwezi hauko mbali vya kutosha.

⁸⁶ Halafu Warusi, wakisema, “Loo, tulimpeleka mtu wa kwanza angani.” Hakika ninatofautiana nao hapo. Huyu mtu alienda angani yapata miaka miwili iliyopita. Nasi tumekuwa na Mmoja angani kwa muda wa miaka elfu mbili, akitujengea makazi tutakayoyaenda.

⁸⁷ Lakini, mnaona, ufanisi wa kujibunia, yale mwanadamu amefanikisha kufanya kwa nafsi yake, hayatafaa kitu.

⁸⁸ Sasa tumejaribu kuwaelimisha watu, kupata kile ambacho tungeita “Watu wa tabaka bora zaidi,” kwa elimu. Seminaru zetu zimewapeleka wahudumu wetu shuleni, ambalo ni jambo zuri, na wakajifunza elimu kwa kuzungumza ipaswavyo, hotuba, na kadhalika, na sarufi bora zaidi. Kwamba, huko ambako tabaka bora la watu wa mjini, wanavyojiita, wangukuja kwenye makanisa haya. Nasi tumejaza kanisa letu na watu hao.

⁸⁹ Sasa, siamini kuna tabaka bora zaidi la watu kuliko watu wa Mungu. Mnaona? Wala Yesu hakutenda kazi juu ya tabaka kama hilo wakati alipokuwa hapa. Yeye aliwaenda wavuvi, wasio na elimu, wasio na kisomo, wasio na maarifa. Na hao ndio Yeye aliowachagua. Na Mungu, kama tu ungaliweza kumfahamu, Yeye hupenda kuchukua kitu ambacho si kitu na kufanya jambo fulani nacho. Hilo linathibitisha kwamba Yeye ni Mungu. Hakuna kitu unachoweza kujivunia. Yeye

huchukua kitu ambacho ni duni, kufanya kitu fulani kwacho. Hilo linathibitisha ya kwamba Yeye ni Mungu.

⁹⁰ Sasa, tulijaribu kufanya jambo hilo basi kwa madhehebu. Tulidhania, labda, kama tungeweza kuyafanya madhehebu yetu kukua. Nasi tulifanya nini, katika kuyaunda madhehebu yetu? Ambayo, ni sawa; sina kitu dhidi yao. Lakini jambo tulilofanya na madhehebu yetu, tulianza tu kulitetea dhehebu hilo, na muda si muda hatukumpa ndugu huyo mwingine blanketi la kutosha kumpa joto. Unaona? Nasi tukajitenga basi. Unaona? Na katika kufanya hivyo, ndipo tulisababisha jambo fulani kutukia miongoni mwetu, ambalo halikupaswa kutukia. Na tunaona ya kwamba jambo hilo halifai kitu.

⁹¹ Hotuba zetu za kiakili, ambazo ni sawa, ila tu laiti ningaliweza kuzitoa. Lakini hilo silo linalohesabiwa mbele za Mungu. Ni Roho Mtakatifu. Mungu kamwe hakuchagua hilo. Alichagua na kuliagiza Kanisa Lake liende likaihubiri Injili. Injili si jambo la kiakili. “Injili haikuja kwa neno tu, bali kwa nguvu na uthibitisho, madhihirisho ya Roho Mtakatifu.” Hayo ndiyo yaliyoileta Injili.

⁹² Hapa si muda mrefu uliopita hapa Chicago, kundi moja la Full Gospel liliitisha mkutano. Nao wakaenda kwenye shule fulani kubwa ya Biblia, nao wakampata msemaji hodari wa kielimu. Na ilitangazwa kote mjini, kuhusu mnenaji huyu hodari kutoka kwenye shule moja fulani kuu, anayejulikana sana, jamani, na digrii zote mbele ya jina lake, mpaka walidhani ya kwamba hilo kweli lingetosha. Na wakati makundi ya watu yalipokusanyika kumsikia mtu huyo, wakati aliposimama huko nyuma ya jengo amevaa suti, ukosi uliopinduliwa, na hotuba yake chini ya mkono wake, akaenda na kuitandaza mahali pale.

⁹³ Na hotuba hiyo, jamani, ilikuwa ni nzuri sana. Hakuna mtu angaliweza kusema neno juu ya hotuba hiyo. Ilikuwa ni kamilifu. Sarufi ilikuwa ni sawa kabisa. Matendo yake mimbarani na tabia zake zilikuwa kamilifu. Hakugugumiza maneno, kubabaika, wala kudorora, kama wengi wetu tunavyofanya. Lakini yeye—lakini yeye. . . Alitoa hotuba yake, kwa ufasaha sana.

⁹⁴ Lakini aliwazia, “Nikiwa na kundi kama hili la watu wasioelimika, nitapanda pale juu na kuwaonyesha vile inavyomaanisha kweli kuwa mhubiri.” Huku kifua chake kikiwa mbele, alipanda juu, amejaa majivuno, na kutoa hotuba hii. Lakini alikuta kwamba hiyo haikukolea kwa umati wa aina hii. Iiruka ikapita juu ya vichwa vyao. Maneno mengi makuu mno, ya majigambo, hawakuielewa.

⁹⁵ Kwa hiyo baada ya kitambo kidogo, wakati alipoona amekosea, alikusanya hotuba yake na kuiweka kwenye mkono wake. Mabega yake yakainama. Kichwa chake kikainama.

Magoti yake yakigongana. Alishuka moja kwa moja chini, mnyenyekevu, ameaibika, akitoka mimbarani.

⁹⁶ Kulikuwako na mzee mtakatifu aliyeketi kule nyuma, akiangalia kote, akamgusa mwingine, kasema, “Kama angalipanda jinsi alivyoshuka, angalishuka jinsi alivyopanda.”

⁹⁷ Kwa hiyo hilo karibu ni kweli, mpaka mtu atakapojua ya kwamba hajui kitu, na atajinyenyekeza mbele za Mungu na kumtarajia Roho Mtakatifu kufanya kazi. Jambo ndilo hilo. Mwanadamu hawezi kufanikisha jambo lolote kwa akili zake. Inambidi kumtegemea Mungu pekee.

⁹⁸ Sasa, mwanadamu akifanya jambo hili, inaonyesha ya kwamba kuna ufanisi mahali fulani, kwa jambo hili kuu la kukombolewa. Na Mungu alifanya ufanisi huo. Alifanya hivyo, na aliufanya rahisi sana: ulikuwa ni kwa imani. Mungu aliwaambia, hapo mwanzo, daima imekuwa ni kwa imani. Leo hii huokolewi kwa matendo, kwa mambo mema, kwa kujiunga na kanisa, kwa kupata elimu. “Unaokolewa tu kwa imani, na hiyo ni kwa neema ya Mungu.” Unaokolewa kwa imani, kwa kuamini yale Mungu ametenda tayari.

⁹⁹ Mungu alitoa ile bendera. Mungu alikupa kitu fulani cha kushikilia, bendera, kama vile bendera ikining’inia.

¹⁰⁰ Na huko Korea, na, loo, huko chini visiwani, wakati wa vita, wakati Wamarekani walikuwa wamewasukuma nyuma Wajapani. Nao wakakimbia kuingia Guam na mahali mbalimbali, mpaka juu ya kilima, kilima kirefu sana wangiweza kupata. Na hapo, huku machozi yakitiririka mashavuni mwao, na wakipiga makelele, waliipandisha bendera ya Marekani, Utukufu wa Kale, kilimani. Walikuwa wameiteka nchi hiyo. Ni ufanisi wa jinsi gani, kuinua bendera hiyo, ya kwamba, “Hii ni mali yetu.” Loo, ilikuwa ni majaliwa ya jinsi gani kwa askari hao, kusimama pale juu ya nchi ambayo walikuwa wameiteka.

¹⁰¹ Ninawaambia, Mungu alilipa Kanisa bendera siku moja, wakati Yesu alipoinuliwa juu pale Kalvari kati ya mbingu na nchi, si mwingine ila ni Mungu, Imanueli, akiimwaga Damu Yake ardhini. Hiyo hapo bendera iliyoinuliwa juu kwa watu, ya kwamba, “Tumeshinda. Tumeshinda. Sisi ni zaidi ya washindi, kwa sababu Yeye alitushindia.”

¹⁰² Sasa tunaona ya kwamba Nuhu, mtu wa Mungu, alikuwa na imani, na Mungu akampa bendera. Na bendera hiyo ilikuwa ni safina. Basi Nuhu akaijenga, kwa imani, kwa kuwa ilikuwa ni amri ya Mungu, kuijenga safina hii kwa ajili ya kumwokoia yeyote atakayeingia ndani yake. Sasa, wakati Nuhu alipoendelea mbele, akaijenga safina, alijua ya kwamba alikuwa akimalizia bendera ambayo Mungu alikuwa amemwambia aijenge. Lolote ambalo Mungu anasema lifanywe, lishikilie, kwa maana ni kweli. Haidhuru ni wenye kudhihaki wangapi waliicheka na

kuidhihakia, Nuhu alijua ya kwamba alikuwa na BWANA ASEMA HIVI.

¹⁰³ Mlinganishe Nuhu na Nimrodi. Nimrodi alikuwa na wazo lake mwenyewe juu ya jambo hilo; naye Nuhu alikuwa na wazo la Mungu kuhusu jambo hilo. Nimrodi alikuwa na kitu angaliweza kushikilia kwa mikono yake; naye Nuhu alikuwa na kitu fulani angaliweza kushikilia kwa mikono yake. Ilikuwa ni bendera, kitu ambacho angeweza kushikilia. Hakika.

¹⁰⁴ Ndipo tunaona ya kwamba, baada ya jambo hilo. Tutazungumza juu ya mtu mwingine upesi, na jina lake lilikuwa ni Musa. Naye alikuwa ni mtu mmoja tu. Lakini angewezaje kamwe kuwakomboa wana wa Israeli kutoka Misri, kutoka utumwani; baada ya yeye kusoma shuleni, alikuwa amefunzwa katika hekima yote ya Wamisri, na akajikuta ameshindwa kabisa? Lakini siku moja, huko mbali kwenye jangwa, Mungu alimkuta, ama yeye alimkuta Mungu. Ndipo Mungu akampa bendera, fimbo kushika mkononi mwake. Ni kitu rahisi jinsi gani, bali ilitenda kazi. “Chukua fimbo hii mbele zako.” Ilikuwa ni bendera. Hiyo, Musa, wakati alipokuwa na fimbo hiyo, alisonga mbele nayo.

¹⁰⁵ Nilikuwa nikisoma si muda mrefu uliopita juu ya David Livingston, niliposimama kwenye kaburi lake huko London. Na watu wengi zaidi hulizuru kaburi la Livingston kuliko kaburi lingine lolote huko Abbey. Ndipo, nilipoisikia hadithi ya Livingston, jinsi alivyoshuka akaenda kule kama daktari na Mkristo. Jinsi alivyowaendea wenyeji, wala asingeweza kuingia, kwa sababu walikuwa zaidi sana ni wakatili.

¹⁰⁶ Kwa hiyo, alimwendea chifu. Naye akasema, huyo chifu akasema, “Kama utakunywa damu ya agano pamoja nami, basi utakuwa mmoja wetu.” Kwa hiyo walichukua divai kwenye kikombe, nao wakatoboa mishipa ya damu ya mmoja kwa mwingine, na kuishikilia juu ya kikombe na kudondosha damu mle ndani, na kuzikoroga, damu hizo mbili pamoja. Ndipo Livingston akanywa nusu yake. Naye yule chifu akanywa nusu yake.

¹⁰⁷ Na kisha wakapeana bendera mmoja kwa mwingine, kwamba walikuwa ni ndugu. Naye chifu akamwomba Livingston koti lake la udaktari, naye akavua koti lake na kumpa huyo chifu. Ndipo basi Livingston akamwomba chifu mkuki wake wa heshima sana.

¹⁰⁸ Basi wakati aliporudi kwenda porini, na hao wenyeji wakamfukuza, wangemchoma mkuki, jinsi angeweza kujisikia vizuri wakati alipoinua bendera hii, ule mkuki wa heshima sana. Na wakati alipouinua, namna hiyo, hao wenyeji wangeanguka chini na karibu wamwabudu kama Mungu, kwa sababu walijua ya kwamba huko ndiko huo mkuki wa heshima sana ulikotoka.

109 Sasa, hiyo ni leo hii. Watu wa siku hizi wanashindwa kutambua ile ishara kuu ambayo Mungu ametupa.

110 Unasema, “Ndugu Branham, je! una nguvu? Laiti ningalikuwa na nguvu.”

111 Hatuna nguvu. Haitupasi kuwa na nguvu. Tuna mamlaka. Si nguvu. Ni mamlaka. Hatuhitaji nguvu. Kristo yuna nguvu. Bali tuna mamlaka. Amina. Kuna tofauti kubwa sana. Yeye Ndiye aliyeshinda. Alishinda na akatupa mamlaka. Yeye yuna nguvu, ila sisi tuna mamlaka, kama tu vile balozi yeyote akienda kwenye nchi nyingine.

112 Hapa, kuwaelezea jambo hilo. Kuna, chini... Ukishuka kwenda hapa kwenye moja ya njia hizi panda hapa Phoenix, yapata saa kumi na moja alasiri. Kuna polisi anayesimama pale. Haya hapa magari yanapita, maili arobaini, hamsini kwa saa. Vema, maskini polisi huyo mdogo huenda asiwe na urefu wa futi tano, anatembea pale, na, mbona, hana nguvu za kutosha kusimamisha moja ya magari hayo. Vema, moja ya magari hayo huenda likawa na nguvu za farasi mia tatu. Vema, yangemchukua tu maskini jamaa huyo mdogo na kumponda, na kuendelea na safari. Lakini hebu na ainue mkono wake mara moja, apige filimbi. Hana nguvu, bali ana mamlaka. Jambo ndilo hilo. Breki zitafungwa, na magurudumu yataalika kweche kweche. Kila kitu kitasimama kwa sababu yeye aliuinua mkono wake, kwa sababu ana mamlaka.

113 Na wakati mwanamume ama mwanamke amevaa silaha zote za Mungu, si nguvu. Ni mamlaka kutoka Juu, wakati anaposema. Pepo watapiga mayowe na breki zitaalika. Hata mauti yenyewe yatatetemeka, na makaburi yatafunguka, kwa mamlaka ambayo Yesu Kristo alilipa Kanisa Lake. Watu wote wanajua jambo hili. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Inueni mamlaka hayo, ile bendera.

114 Mkono wake umeinuliwa, huku amevaa glavu yake nyeupe, na kila gari litasimama. Yeye hana nguvu za kutosha, labda, ku-kuisimamisha baiskeli. Lakini ana mamlaka ya kusimamisha chochote kinachopitia humo barabarani. Sababu kwa nini? Sheria yote ya Phoenix iko nyuma yake.

115 Na Mkristo aliyekufa, na kuzikwa, na kufufuka pamoja Naye katika ufufuo Wake, katika ulimwengu wa Roho! Unaona, “Kama tumekufa pamoja Naye, basi pia tumefufuka pamoja Naye,” kwa kuwa Mwili huenda mahali Kichwa kilipo. Naye ndiye Kichwa, na huu ndio Mwili. Na si kwamba utakuwa, bali, “Sasa tumeketi pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu,” huku kila nguvu ya ibilisi imeshindwa na iko chini ya miguu Yake. Mamlaka! Mamlaka, hiyo hapo bendera. Huo ndio mkono unaoinuliwa, ndio ulio muhimu.

116 Musa alishuka akaenda Misri. Kulikuwako na bahari kubwa huko mbali. Akainua bendera, na ni jambo gani lililotukia?

Ziligeuka zikawa damu. Ikainuliwa juu ya nchi; vyura, chawa, viroboto. Jua likakataa kuwaka. Mauti yakaipiga nchi. Kwa nini? Yeye alinua bendera ya hukumu ya Mungu.

117 Na wakati tunapoinua bendera ya hukumu ya Mungu, kama mwaminio katika Kristo, pamoja na maisha yaliyosulubiwa kwa nafsi yako na mawazo yako mwenyewe, na kufufuliwa, na Neno Lake limefanywa hai miongoni mwenu, kila pepo hana budi kulia kwa Hilo. Hiyo ni kweli. Maana, inamwakilisha Kristo. Mnaona? Yeye alikufa. Ndiye aliyeiinua bendera.

118 Na Musa akiwa na fimbo yake, ilionekana kama kitu kidogo sana, bali ilikuwa ni fimbo. Nayo ilikuwa ndiyo bendera ya Mungu kwa Misri, fimbo yake ya hukumu, nayo ilileta hukumu. Mungu daima hutoa kitu ambacho unaweza kukiangalia, kitu ambacho unaweza kukishikilia kwa mkono, kitu ambacho unaweza kuthibitisha, kitu ambacho ni cha kweli, baada ya wewe kumkubali Yeye. Wale majusi, Majusi . . .

119 Tunasoma, Petro alisema ya kwamba aliona ya kwamba Mungu alikuwa yupo, angechukua taifa lolote la watu, mtu yeyote aliyemwamini.

120 Wale majusi, walikuwa wakiitazamia nyota iinuke kutoka kwa Yakobo, nyota fulani kutoka kwa Yakobo. Nao walipewa bendera. Yesu alipozaliwa katika Bethlehemi ya Yuda, majusi walitoka India wakiifuata nyota. Loo, jamani! Ati nini? Bendera, dhahirisho, hakikisho, hakikisho la kimbinguni.

Ewe usiyeamini, ningetaka uone jambo hili.

121 Si kwamba kila mtu anapaswa aione. Hakuna mtu aliyeiona hiyo nyota isipokuwa hao watu watatu. Alipitia juu ya kila jumba la kuchunguzia, thibitisho halisi lililo hai, bendera ya kuwaongoza kwa Kristo. Hakuna mtu aliyeiona ila wao.

122 “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Hata hivyo mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi daima, hata ukamilifu wa dahari.” Ile bendera, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele,” bendera ya kweli ya Mungu. Asiyeamini huenda asiione.

123 Yesu alisema pia, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Ingekuwa ni kitu gani? Ingekuwa ni ishara, bendera.

124 Wakati mmoja Yeye aliombwa, “Jalia mwanangu aketi kwenye, mmoja mkono wa kuume, mmoja mkono wa kushoto.”

125 Yeye akasema, “Je! mwaweza kukinywea kikombe ninyweacho Mimi? Mwaweza kubatizwa ubatizo nibatizwao Mimi?” Roho Mtakatifu yeye yule aliyekuwa juu Yake pasipo kipimo, anakuja juu ya Kanisa Lake kwa kipimo, bali ni Roho Mtakatifu yeye yule, Mungu yeye yule. Ni bendera.

126 Sisi ni bendera za Mungu kwa ulimwengu. Hiyo ndiyo sababu daima ninalikemea kanisa la Kipentekoste,

kuwafuatilia, jinsi wanavyoishi. Hiyo ndiyo sababu ulimwengu hauwezi kumwona Kristo, ni kwa sababu tunaachilia mambo. Tunaondoka kwenye jambo hilo.

¹²⁷ Wakati wanawake wetu wanapovalia na kutenda kama ulimwengu; wakati wanaume wetu wanapotoka nje, na mizaha michafu, na kuvuta sigara, na kufanya yasiyofaa kama hao wengine; wameoa mara nne ama tano, na kila kitu; wanawavuta, wanawaingiza kanisani, na vitu kama hivyo. Mbona, la. U—ulimwengu hauamini kwamba mmelipata.

¹²⁸ Hebu nikwambie, ndugu, wakati umekufa, na uhai wako umefichwa katika Kristo, kwa Mungu, na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu, na Mungu anakuinua katika ulimwengu wa Roho, utakuwa bendera ya kwamba kazi ya Mungu imefanywa ndani yako.

¹²⁹ Yesu alisema katika Marko 16, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Ni bendera ya aina gani? Mtu mashuhuri mwenye kiburi? La. Unyenyekevu. Utimilifu wa Mungu katika Kristo Yesu ulimfanya atembe kama mkulima mdogo mnyenyekevu, ulimfanya aitawadhe miguu ya wanafunzi Wake, hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake.

¹³⁰ Baadhi yetu tunaojiita Wakristo, tukienda mahali fulani, inabidi kupata yaliyo bora sana nchini; inabidi tuhakikishiwe fedha nyingi kiasi fulani, vinginevyo hatutaenda, mwinjilisti. Wachungaji wengine hawataenda kwenye kanisa fulani isipokuwa ni mahali pakubwa pa tabaka la juu. Loo, jamani!

¹³¹ Tunahitaji tukio lingine kama aliloona Paulo wakati alipokuwa akienda zake Dameski. Paulo aliona ile bendera imeinuliwa! Ndipo akasema, “U nani Wewe, Bwana?”

Akasema, “Mimi ni Yesu.”

¹³² Tunachohitaji usiku wa leo ni Nguzo nyingine ya Moto iking’inia juu ya kanisa tena usiku wa leo, ili macho ya watu yaliyopofushwa yangefunguliwa na yangeweza kuiona.

¹³³ Yesu angali anaishi na anatawala, ile bendera. Sasa, Yeye ndiye ninii. . . Mungu aliyetupa sisi bendera hii. Ni bendera ya Milele.

¹³⁴ Kumbukeni ya kwamba bendera zote za Kirumi, bendera zote za Nimrodi, zote za Babeli, na hizo zingine zote, zimepondwapondwa na kuangamizwa. Tunazijua tu kwa historia. Nilisimama huko Roma, ambako Makaisari wakati fulani waliutawala ulimwengu, nawe ingekubidi kuchimba chini futi ishirini chini ya ardhi, kupata mahali ambapo ikulu yao ilikuwapo. Nilisimama huko Misri walikokuwa Mafarao, na imeishia na kugeuka kuwa mavumbi.

¹³⁵ Ndugu, lakini kuna bendera ambayo Mungu aliipata siku moja, kwa kumwinua Yesu Kristo kutoka kwa wafu, na kumtuma Roho Mtakatifu katika Kanisa Lake. “Na mbingu

na nchi zitapita, bali Neno Lake halitapita kamwe.” “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.” Kwa nini? Bendera iliyo hai ipo Kanisani: bendera, isiyoshindwa, thibitisho lililo kamilifu, kitu fulani unachoweza kukishikilia kwa mkono, kitu ambacho ungeweza kukiangalia.

¹³⁶ Unaona hapa, mvulana huyu mdogo, mvulana Williams hapa, alisimama na kushuhudia jinsi baba yake na mama yake walivyokuwa wamemwombea, na kwa ghafla akaiona ile bendera. Jambo fulani lilitukia. Aliona. Aliiaga ile nyumba ya kale ya udongo, na ndipo akaenda kukimbia kwenye Kilimia Cheupe, kama vile ndugu huyu alivyosema.

¹³⁷ Wakati wanadamu wanapoweza kuona jambo hilo! “Kama nikiinulia juu ya nchi, nitawavuta watu wote Kwangu. Ninzi ni mashahidi Wangu. Mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, Yuda, Samaria, na pande za mwisho za dunia. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Katika Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya, watahika nyoka, watakunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru, wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.” Ile Bendera. Hebu nichukue lingine juu ya hilo, kulitilia muhuri. “Hivyo watu wote watajua ninzi ni wanafunzi Wangu, mkipendana ninzi kwa ninzi.” Mnaona? Hamwezi kuchukua sehemu yake. Inawabidi kuchukua yote. Wala haiwezi kutiwa muhuri mpaka yote ya Hiyo imekuja. Hiyo ni kweli.

¹³⁸ Katika nchi ile ya kale, zamani za kale, muhuri kwa kawaida ulikuwa ni pete. Mtu ambaye asingeweza kuandika jina lake, alikuwa tu na pete, naye akaitia muhuri. Ninzi yake, yoyote aliyoandika, mbona, yeye angeninzi tu, badala ya kuandika jina lake, alitia muhuri juu yake. Lilikuwa ni kosa la kufungwa gereza ni kunakili muhuri huo wakati wowote.

¹³⁹ Sasa, siku hizi, Mungu ana Muhuri, na ni hukumu ya kifo kunakili Muhuri huo. Sikilizeni, enzi Walutheri, Wamethodisti, Wabaptisti, Waprebiteri na Wapentekoste, msijaribu kuunakili.

¹⁴⁰ Tulieni kimya, naye Mungu atauweka Huo juu yenu. Na ndipo mtakapokuwa bendera, mfano wa Ukristo, na uanaume na uwanawake. Muhuri wa Roho Mtakatifu, bendera ya Mungu, imepigiliwa kwako mpaka unaonekana, unatenda, unatembea, unazungunza Injili kila mahali uendapo. Hakuna kidole unachoweza kuelekezewa. Hiyo ni kweli.

¹⁴¹ Mungu amefanikisha jambo hilo kwa mauti, kuzikwa, na kufufuka kwa Yesu Kristo, “Kwa kuoshwa kwa maji ya Neno.” Kwa Damu Yake leo tumeoshwa na kusafishwa, tukapewa baraka hizi kuu.

¹⁴² Mnaona, tunashangaa kwamba Yesu alikuwa ni nani, kama tukisema alikuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa,

kile alichokuwa jana, ndicho alicholeo, na atakuwa milele, bendera ile ile.

¹⁴³ Tunaona kile bendera hiyo ilichokuwa kwa watu hao, kujua kama Yeye alikuwa ni bendera ya kweli tuliyotarajia kuwa ije. Tunaona katika Maandiko, ambapo ndani humo kamwe Yeye hakudai kufanya lolote. Hakudai kamwe. Yeye alisema, “Si Mimi nikitendaye hizo kazi. Ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu. Ndiye atendaye kazi hizo. Amini, amini nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno, bali kile amwonacho Baba anakifanya, ndivyo anavyofanya Mwana vile vile.” Ni kile alichomwona Baba akifanya. Kwa maneno mengine, Yeye aliona jambo kwa ono, jambo lililotukia.

¹⁴⁴ Tunaona, mwanamke mmoja aligusa vazi Lake. Akageuka akamwalia, na kuongea naye. Alikuwa akitokwa na damu, nayo ikakoma. Imani yake ilimwoko.

Yule mwanamke kisimani. Kasema, “Nenda, kamwite mume wako.”

Akasema, “Sina mume.” Kasema, “Vema, sisi. . .”

“Ulisema kweli, kwa maana umekuwa na watano.”

¹⁴⁵ Wakati aliposema jambo hilo, alisema, “Bwana, tunajua ya kwamba yuaja Masihi, Ambaye anaitwa Kristo. Wakati atakapokuja, atatwambia mambo haya.” Mnaona?

Hiyo hapo bendera. Yeye akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

¹⁴⁶ Loo, ndugu, mtungi wa maji uliachwa. Alikuwa amepata chemchemi iliyojaa Damu iliyotolewa kwenye mishipa ya damu ya Imanueli. Alikuwa amepata Chemchemi ya wokovu. Alikuwa amepata Chemchemi. Alikimbia kwenda mjini. Mnaona? Alikuwa akiwaelekeza wanaume kwa furaha. Akasema, “Njoni, mwone Mtu tuliyempata. Angalieni Mtu aliyeniambia mambo yote niliyofanya.”

¹⁴⁷ Mwangalie Andrea, ambaye nilihubiri juu yake jana usiku kule. Jinsi ambavyo, mara baada ya kukaa usiku kucha pamoja na Yesu, na kupata kwamba huyo kweli alikuwa ni shahidi wa Mungu, huyo alikuwa ni Masihi, hakuenda, akasema, “Simoni, njoo, nisaidie kutatua jambo hili.” Alijua ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi.

¹⁴⁸ Na mara alipokuja mbele Zake, Yeye alimwambia kwamba alikuwa ni nani, na jina la baba yake lilikuwa ni nani, naye Petro akajua ya kwamba hilo ndilo lingetukia.

¹⁴⁹ Filipo alifanya jambo lilo hilo. Na, loo, kuendelea, na kuendelea, na kuendelea, ile bendera.

¹⁵⁰ Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.”

151 Sasa angalia. Tunatumwa. Sikilizeni hapa, enyi marafiki, ninyi nyote. Ninasema na ninyi watu sasa, hiyo ni sasa hivi, kwa watu watakaoombewa. Sikilizeni jambo hili.

152 Wewe ni shahidi. Umeokolewa, na unajua nguvu za Mungu ni nini, umegusa bendera hiyo. Umeshikilia kitu fulani, kitu fulani, sio mnara wa Nimrodi. Wala si—si aproni ya mtini ya Adamu. Lakini ni ahadi ya Mungu, kwamba, “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe.” Ni jambo ambalo unaweza kulishikilia kwa mikono. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Kama wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Ni bendera, bendera halisi.

153 Na kwenu ninyi watu, kama kuna mmoja hapa, ambaye kamwe hajaikubali bendera hii, ambaye hajui ni kitu gani kinachowafanya watu hawa kulia, na kupaza sauti, na kucheza; na jinsi linavyowafanya wanawake hawa kuachilia nywele zao zikue, na kuacha kuvaa hizo nguo za kale chafu, na—na kuonekana wenye kuvutia kimapenzi mbele ya wanaume, na mambo kama hayo, yule pepo mchafu wa kale amewatoka.

154 Usiniambie. Unaweza kuwa safi kama yungiyungi kwa mume wako; lakini utakapokuja kwenye Kiti cha Hukumu, utajibu kwa kufanya uzinzi. Hiyo ni kweli. Biblia ilisema. Yesu alisema, “Mtu akimwalia mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” Na kama ukivaa ukajianika mbele za wanaume, wewe una hatia, hata mwanamume asipokugusa. Wakati mwenye dhambi huyo atakapowajibika kwa ajili ya uzinzi wake, wewe ndiwe uliyezini. Umejianiwa mwenyewe. Naam, bwana. Ndugu, dada, huenda ukafikiri kwamba hili ni la mtindo wa kale.

155 Nilikuwa na mhudumu si muda mrefu uliopita, aliyesema, “Utaiharibu huduma yako, Ndugu Branham.”

156 Nikasema, “Si yangu. Ni Yake. Na hilo ni Neno Lake, na hilo ndilo alilosema.” Ninaamini Hilo. Naam, bwana. Naam, bwana. Kweli.

157 Kwa hiyo wakati unapomwona mmoja wa hao wanawake akijiweka sawa na Mungu, utamwona akitokea kama mtakatifu. Utamwona akitenda tofauti. Kutakuwa—kutakuwako na tofauti maishani mwake. Utakatifu utanena kila mahali. Yeye atakuwa ni mama wa heshima.

158 Mwangalie mwanamume huyo, huyo mlevi huko nje barabarani, akiyumbayumba, nzi wa baa, na mdomo wake umejaa mayai ya nzi, kutokana na kutapika, kutokana na wiski na bia na takataka kama hizo. Hebu ashuke aende madhabahuni na kuishika bendera hiyo siku moja, nami ninawaambia yeye atakuwa ni bendera kwa Mungu, na kumbukumbu ya nguvu za kuokoa za Yesu Kristo. Naam, bwana. Bila shaka atakuwa.

159 Nilisimama hapa chini, hivi majuzi, hapa kwenye mitaa ya Phoenix na kuona mvulana mdogo, mweusi amesimama pale.

Jamaa mdogo, hakuna mtu aliyekuwa akimjali. Alikuwa na Biblia yake kwenye mkono wake, na kila mtu aliyekuwa akipitia pale, alikuwa akiwaelekezea Injili, kwa bidii jinsi alivyoweza. Nikasema, “Bwana Mungu na ashukuriwe. Loo, jamani! Ipazie sauti, ndugu. Iendeleze mbele tu. Hilo ni sawa, ukimwinua Yesu Kristo.”

¹⁶⁰ Loo, kama hamumjui usiku wa leo, enyi marafiki, mpokeeni. Si mfanye hivyo, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa dakika moja tu kwa ajili ya maombi? Ninasikitika, wakati unapita mbio.

¹⁶¹ Ninataka kuuliza, kwa dakika moja tu, je! kuna mwenye dhambi hapa usiku wa leo asiyemjua Kristo wala hajapokea bendera hii?

¹⁶² Kama ulijaribu kufanikisha, kusema, “Sasa, Ndugu Branham, sasa hebu kidogo tu. Mimi ninatekeleza ile kanuni ya msingi.” Ndugu, kama hilo lingalisimama, isingemlazimu Yesu kufa. Unasema, “Ndugu Branham, nimekuwa mfuasi wa kanisa linalosifika sana.”

¹⁶³ Hilo ni sawa, ndugu yangu. Ninathamini jambo hilo, na ninathamini kutekeleza kwako ile kanuni ya msingi. Ninathamini kushika kwako zile amri kumi. Lakini kama ile kanuni ya msingi, kujiunga na kanisa, ama lolote la mambo hayo, lingalikuokoa, Yesu alikufa bure. Yesu alisema, Yeye Mwenyewe, katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 3, “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hataingia kamwe.”

¹⁶⁴ Maisha ni kama jani linaloning’inia mtini. Baada ya kitambo kidogo uhai huliacha jani hilo, na kurudi kwenye mizizi yake. Hilo jani linaanguka. Uhai huo unazikwa katika mizizi mpaka majira ya baridi kali yapite. Katika msimu wa kuchipusha inaleta uhai mwingine, jani lingine.

¹⁶⁵ Hiyo ndiyo njia ya Mkristo aliye kwenye Mti wa Uzima. Ganda hili hapa la kale huenda likaharibika. Hiyo ni kweli. Lakini uhai unamrudia Mungu aliyettoa. Mnaona? Kama Mungu akikupa uhai wako, umezaliwa mara ya pili, kuna uhai mmoja tu unaoweza kuishi, na huo ni Uhai wa Mungu ndani yako. Na kama uhai huo umo ndani yako, basi utaenda tu mahali ulikotoka, kurudi kwa Mungu, upate kurudi katika ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu, ukiwa na jani jipya, ama uhai mpya, ama ninii mpya—ama mwili mpya ambao kamwe hautanyauka wala kuharibika.

¹⁶⁶ Misimu yetu huonyesha ya kwamba Mungu yu pamoja nasi, ya kwamba Mungu yupo hapa. Yeye aliamuru maumbile. Sasa, kama hujapata kamwe kupokea uhai huo, kama maskini jani hilo lingeanguka usiku wa leo, maskini jani hili ulilo hapa duniani, unajua kamwe halingefufuka tena; kama hujazaliwa mara ya pili, hujapokea ile bendera moyoni mwako, ule ushahidi, Roho Mtakatifu. Si la kuwazia tu. Huwezi kuwazia jambo hilo.

¹⁶⁷ Nilizungumza mahali fulani hivi majuzi usiku, na kusema, “Vipi kama wanafunzi wangalingojea siku tisa, na kusema, “Tutamkubali kwa imani, ya kwamba tuna Roho Mtakatifu, na tuendelee?”” Wasingalimpata. Mnaona? Walikaa pale mpaka walipojua Yeye alikuwapo. Jambo fulani lilikuwa limetukia, jambo fulani ambalo wangaliweza kulishikilia kwa mikono yao, waseme, “Hili ndilo.” Kama tu vile Nuhu angaliweza kusema, “Hili ndilo.” Kama tu Musa angaliweza kusema, akiwa na fimbo mkononi mwake, “Hili ndilo.”

“Utakwenda kushinda namna gani, Musa?”

“Kwa fimbo hii nitashinda. Hivyo ndivyo nitakavyoshinda.”

¹⁶⁸ Na kwa Yesu Kristo, kwa Roho Mtakatifu, nimeshinda. Nimeshinda, kwa kuwa Yeye alishinda kwa ajili yangu. Na sasa mimi . . . Uhai wangu umekufa, na kufichwa ndani Yake, na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu. Uko pale.

¹⁶⁹ Kama huna tukio hilo usiku wa leo, ewe rafiki mwenye dhambi, je! waweza kuja wakati tukiinamisha vichwa vyetu kwa dakika moja tu?

¹⁷⁰ Baba yetu wa Mbinguni, sasa ninawakabidhi wasikilizaji Kwako. Huenda kukawa na mtu mpotovu hapa ambaye huenda asipate nafasi tena. Ndio kwanza tusikie kwenye simu, dakika chache zilizopita, ama muda mfupi uliopita, Ndugu Tommy Hicks, mtumishi Wako wa thamani. Ndugu yake, ambaye alikuwa amemlilia, akamsihi, majuma machache tu yaliyopita, hata akamtumia barua, na kusema, “Ndugu, mpokee Kristo.”

¹⁷¹ Lakini alikuwa akipata fedha nyingi sana, akajinunulie makazi ya dola laki moja, Kadilaki mpya, hakuwa na wakati wa kufanya jambo hilo. “Nafikiri nitafanya hivyo baadaye, Tommy.” Lakini muda umekwisha kabisa sasa. Yalimshika, huko chini Mexico.

¹⁷² Ee Mungu, turehemu. Jalia watu wajue ya kwamba hakuna kurudi tena kujaribu tena. Hii ndiyo nafasi ya pekee. Wala mauti hayaibadilishi nafsi; yanabadilisha tu makazi yake.

¹⁷³ Sasa, Baba, ninaomba, kama kuna mtu hapa anayejua ya kwamba wameumbwa kwa utu huu wa utatu, wa nafsi, mwili, na roho pia, ya kwamba ndani ya mwili wanamoishi kuna roho. Ndani ya nafsi inayowaongoza kuna roho. Ndani ya zile hisi tano kuna roho. Na kama roho hiyo si Roho ya Mungu, wakati huu mwingine unapoharibika, hauwezi kufufuka tena. Lakini, Mungu, ninakuomba, ya kwamba watakupokea Wewe sasa, na kushika bendera hii nzuri ya Roho Mtakatifu moyoni mwao na waokolewe usiku wa leo.

¹⁷⁴ Na wakati tumeinamisha vichwa vyetu, kama kuna mtu yeyote angetaka kukumbukwa, inua mkono wako sasa, useme, “Niombee, ndugu, mhubiri.” Mungu akubariki. Mungu

akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe, dada. Vizuri sana. Mtu mwingine? Sasa, usione haya.

¹⁷⁵ Endeeleni tu kuomba, Wakristo wote. Watu hawa wanaoinua mikono yao.

¹⁷⁶ Mungu akubariki, msichana. Mungu akubariki, dada. Mtu mwingine? Sema, “Nikumbuke, Ndugu Branham. Mimi, sasa ninaamini. Ni—ninaamini tu, kwa namna fulani. Ninaamini tu.” Mtu mwingine? Mungu akubariki. Mungu akubariki, upande huu. Ubarikiwe, huko nyuma. Hilo ni zuri.

¹⁷⁷ Sasa, hao ni watu walioinua mikono yao. Wanaamini jambo hilo. Madhabahu yamejaa watoto waliosimama. Wako kila mahali, kila mahali. Si lazima uwe na madhabahu. Moyo wako ndio madhabahu. Moyo wako ndipo Mungu anapokuja.

¹⁷⁸ Nilikuwa nikisoma, hivi majuzi, katika historia, *Kanisa Linalosafiri, Wazee wa Nikea*, kilichoandikwa na Broadbent, ambapo, katika kanisa la mwanzoni, hata hawakuwa na mapambo yoyote, hata hawakuwa na madhabahu. Kwa sababu, makafiri, wakiongoka, walikuwa wakisujudu madhabahuni. Walikuwa tu na maskini jengo tupu la kale ambamo waliketi kwenye ubaba wa miamba. Waliinua mikono yao baada ya mtu mcha Mungu kutoa ujumbe. Nao waliinua mikono yao na kumsifu Mungu. Walipenda hayo matokeo ya Roho Mtakatifu kuwasafisha. Hilo lilikuwa ni kanisa la mwanzoni katika nyakati za Irene na Martin, na kadhalika, mara baada ya kifo cha Bwana Yesu, wakati kanisa lilipokuwa likiendelea, kabla halijaingia katika Ukatoliki. Loo, hilo ndilo tunalopenda.

¹⁷⁹ Sasa, wewe uliye hapa fanya madhabahu hayo moyo wako sasa, na useme, “Ingia, Bwana Yesu.” Nitakuombea.

¹⁸⁰ Bwana Yesu, ninatumaini ya kwamba, nikiharakisha upesi sana, nikiyatupa maneno haya pamoja, nikijitayarisha sasa, nasi tunangojewa kuona yale utakayofanya katika mstari wa maombi, bila kujua utafanya nini hasa. Lakini, hata hivyo, kumekuwako na angalau mikono dazan moja iliyoinuliwa, ya vijana na wazee, ambao wanatamani kukujua Wewe, Baba, wanaotaka sana kupata huo Uzima wa Milele. Jalia liwe halisi kwao sasa hivi. Tujalie, Bwana. Jalia Roho wa thamani wa Mungu azilowanishe nafsi zao sasa hivi na kuwafanya viumbe vipya katika Kristo.

¹⁸¹ Na sasa, Baba, ninaomba ya kwamba katika mstari wa maombi ya kwamba utajionyesha Mwenyewe wazi sana mbele ya wasikilizaji hawa usiku wa leo kwa kuwaponya wagonjwa, hivi kwamba wataondoka hapa wakisema kama wale waliotoka Emau, “Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu?” Kwa sababu, waliona jambo fulani likifanywa, hao watu huko Emau, hao ndugu. Walikuwa wametembea siku nzima, Kleopa na hao wengine, wakizungunza Naye, lakini hata hivyo hawakujua kwamba Yeye alikuwa ni nani. Lakini wakati alipofanya jambo

fulani jinsi alivyofanya kabla ya kusulubiwa na kuzikwa Kwake, walijua alikuwa amefufuka katika wafu. Utafanya tena usiku wa leo, Baba? Tujalie, tunaomba.

¹⁸² Sasa tunaomba ya kwamba utawachukua watu hawa wa thamani, uwape Uzima wa Milele. Jalia, kama hawajapata kubatizwa, jalia washike njia waende kwenye nyumba ya mchungaji ama mahali fulani na wakabatizwe, wakiliitia Jina la Bwana. Nami nakuomba Wewe uwajaze na Roho Mtakatifu. Na jalia tuwalaki Utukufuni, katika nchi bora, ambako mkutano wa usiku huu utaletwa hukumuni. Tunalikabidhi Kwako sasa, katika Jina la Yesu. Amina.

Nampenda, nam- . . .

Sasa, baada ya Ujumbe huo wa kukatakata sana, hebu na tuabudu tu sasa.

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

¹⁸³ Hivi hamuupendi huo? Wote ambao . . . Ninyi ambao mlikuwa Wamethodisti, inueni mikono yenu; Wabaptisti, Wapresbiteri, Wakatoliki. Sasa, wote waliozaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, inueni mikono yenu, kama ninyi ni Wamethodisti, Wabaptisti, ama Wakatoliki, ama chochote kile. Hiyo si ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

¹⁸⁴ Sasa, tunapouimba tena, kwa utamu sana, wakati dada anapotupa sauti yake sasa. Hivi hamuupendi huo? Loo, jamani!

¹⁸⁵ Mwajua, utakapofika Mbinguni, na kuingia katika jumba lako kubwa na kuangalia kule chini, utaona mahali pangu padogo kule chini. Moja ya asubuhi hizi, utanisikia nikitoka, nikiuimba, utajua nimefika Nyumbani. Amina. Ninaupenda tu huo. Vema.

¹⁸⁶ Sote pamoja sasa. Usiweke tu . . . Kuwa tu mwenyewe. Ninapenda uimbaji mzuri wa kipentekoste. Nanyi je? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sipendi sauti iliyofunzwa kupita kiasi, mwajua, inayolia, na kushikilia pumzi yao, na kuwa bluu usoni, na unajaribu tu kujiwekea kitu fulani. Na—napenda uimbaji mzuri, uimbaji halisi tu, huru. Sasa kila mtu, pamoja, pamoja na maskini kwaya hii ndogo, pamoja sasa. Sote pamoja sasa.

Nampenda . . .

Na tufumbe macho yetu

. . . Nampenda,
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

¹⁸⁷ Sasa, kwa utamu kabisa, tunapoimba tena. Hebu tugeuke na kupeana mikono na mtu fulani aliye karibu nawe, mbele na nyuma, sasa. “Na . . .” Ninyi nyote wasafiri, wasafiri, wageni kwa ulimwengu. Mkatoliki, peana mikono na Mprotestanti. Mprotestanti, peana mikono na Wamethodisti. Wamethodisti, na Wabaptisti, Wapentekoste. “Alinipenda . . .” Kanisa la Mungu na Waassemblies. Waassemblies, na wa Umoja. Loo!

Kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Sasa huku tumemwinulia mikono yetu.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari

Sasa, kwa unyenyekevu, hebu na tuinamishe vichwa vyetu na kuuvumisha.

¹⁸⁸ Baba, tunaungama dhambi zetu, wakati Neno lingali linapandwa ndani ya mioyo ya watu, ile bendera. Wengi wao wamejifunza hilo muda mrefu uliopita. Tembea miongoni mwetu, Baba. Umewaokoa waliopotea. Sasa waponye wagonjwa, ili kwamba ijulikane ya kwamba Neno Lako halitarudi Kwako bure. Litatimiza kile lililoahidiwa. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda*—Mh.]

¹⁸⁹ Kadi za maombi sasa, tukianza na namba moja, anzeni kusimama karibu na madhabahu namna *hii*, hapa. Maombi . . . Ngojeni. Kwa hiyo afadhali niwaite, mmoja mmoja, kusiwe na kutatanika. Kadi ya maombi namba moja.

Naomba uendeleo kuucheza wimbo huo, dada.

¹⁹⁰ Ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja? Papa hapa. Namba mbili, namba tatu. Vema. Tatu. Namba nne, namba tano, namba sita, namba saba. Endeleeni kutoka moja kwa moja, na mje moja kwa moja huku, simameni tu moja kwa moja *hivi*.

¹⁹¹ [Ndugu Branham anaanza kuvumisha, *Nampenda*—Mh.] “Na . . .” Dumisheni tu roho wa maombi sasa, kwa utamu, kwa kimya.

Kwani alinipenda . . .

¹⁹² Nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane.

Kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda*—Mh.]

Sasa wengine wenu nyote mlio na kadi za maombi.

Alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini . . .

¹⁹³ [Ndugu Billy Paul Branham anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Ndiyo, mwanangu.

¹⁹⁴ Loo, si Yeye ni wa ajabu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vumisheni huo. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda.*]

Nampenda, na . . .

Mnausikia huo? Unasikika kama wimbo wa Malaika, mnaona.

. . . alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

¹⁹⁵ Huo unasikika mtamu? [Kusanyiko linasema, “Amina.” Ndugu Branham anavumisha *Nampenda*—Mh.]

Hamsikii kengele sasa zikilia?
Hamsikii Malaika wakiimba?
Ni Yubile ya utukufu haleluya.
Kwenye umbali huo mtamu milele, (Mungu ahimidiwe!)
Ng’ambo tu ya mto unaometameta,
Wakati watakapozipiga hizo kengele za furaha
kwa ajili yako na yangu.

¹⁹⁶ Sasa, siwezi tu kuachana na jambo hilo. Loo, ninapenda jambo hilo. Ninakumbuka mwanangu, Billy, wakati mama yake alipokufa. Masaa machache, maskini dada yake mdogo akafa. Niliwaweka wote wawili pamoja, huko juu ya kilima, na kuwazika. Nikapanda kwenda kule, na kuketi chini. Maskini hua wa kale alikuwa akiketi huko nje na kulia. Kwa kweli nilidhani huenda ikawa ni nafsi yao isiyopatikana na mauti ikirudi, ikisema nami. Nilikuwa nimevunjika moyo sana. Na ilionekana kana kwamba, nilipokuwa nikishuka kuja kupitia kwenye ile misonobari, kulikuwa na mnong’onezo, kitu kama hicho.

Kuna Nchi iliyo ng’ambo ya mto,
Tunayoiita tamu milele,
Nasi tunaweza kufika tu kwenye pwani hiyo
kwa imani . . .

Hiyo si ni kweli, enyi marafiki? E-nhe! Jamani!

Mmoja mmoja tutafika kwenye hilo lango,
Pale tukaishi pamoja na wasiopatikana na
mauti,

Si litakuwa ni zuri sana watakapofanya jambo hili?

Watakapozipiga zile kengele za furaha kwa ajili yako na yangu.

¹⁹⁷ Sasa, enyi marafiki, juu ya uponyaji wa Kiungu, hakuna—hakuna mtu anavyeweza kukuponya, si zaidi ya vile mtu yeyote anavyoweza kukuokoa; kwa sababu uponyaji na wokovu viko kwenye wakati uliopita. Wakati Yesu Kristo alipokufa pale Kalvari, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu. Kwa mapigo yake sisi tuliponywa.” Ni kazi iliyomalizika. Sasa, jambo pekee unalopaswa kufanya, kupokea ama wokovu wako ama uponyaji wako, ni kukubali yale Kristo aliyokutendea.

¹⁹⁸ Kama nilivyosema, hivi majuzi usiku, hebu na tumwangelie Mungu kidogo tu, huko nyuma kabisa katika Umilele, wakati ninii Yake. . . wakati majua bilioni laki moja yangeonekana meusi Kwake, wakati Malaika walionekana wachafu mbele Zake. Huyu ni Yehova. Ndipo akawa mtoto mchanga, kwenye lundo la samadi, katika hori. Huyu angali ni Yehova. Naye ndiye huyu hapa usiku wa leo. Kupitia neema Yake na kwa Damu Yake, Yeye analisafisha Kanisa Lake na kutuweka tayari kwenye nafasi ya kupokea baraka hizi zote ambazo Yeye alizilipia kwa ajili yetu.

¹⁹⁹ Sasa hapa pamesimama mstari wa watu. Sijapata kumwona yeyote wao maishani mwangu, nijuavyo mimi.

²⁰⁰ Sasa, wengi wenu wamekuwa kwenye mikutano yangu na wanajua utambuzi ni kitu gani. Ninyi nyote mnajua hilo. Sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Tunajua hilo. Nimekuwa nao tena na tena, na tena na tena. Hiyo ni karama. Hiyo haimfanyi Roho Mtakatifu ndani yangu kuwa mkuu kuliko mtu mwingine yeyote. Hiyo ni karama tu, kufanya kazi na Roho Mtakatifu. Mnaona?

²⁰¹ Haidhuru kama ni maskini mke nyumbani, ama mvulana mdogo, ama mlevi huko nje ambaye ndiyo kwanza aokoke na kujazwa na Roho Mtakatifu, yeye yuna Roho Mtakatifu yeye yule ambaye yeyote wetu aliye naye. Naam. Lakini Mungu hutoa karama, pamoja na Roho huyu Mtakatifu, kufanya kazi. Ni dhihirisho, kuinua bendera. Ati nani, mhubiri? La. Kumwinua Kristo.

²⁰² Sasa, sijui ni jambo gani lililotokea. Nilipokuwa mvulana mdogo. . . Mnajua hadithi yangu. Ndiyo kwanza niwaombe watu. Hakuna kitu ninachofanya ila kuomba, kuwawekea mikono, wangepona. Mnaona? Kwa hiyo ningefanya nini? Si mimi pekee ninayeomba, bali angalia wengine wanaoomba. Kila mtu anaomba. Mnaona? Na, ninii tu, ninaamini hilo. Hivyo tu ndivyo ninavyojua kufanya. Ninaliamini.

²⁰³ Sasa, sina elimu, sina elimu yoyote. Nami nafikiri Bwana alinipa tu karama ndogo ya kufanya kazi nayo. Na—na sasa, wakati Yesu aliposema, wakati alipokuwa hapa duniani,

mambo aliyofanya, sisi nasi tungeyafanya. Na kama hilo ndivyo lilivyo. . .

²⁰⁴ Naye alikuwa ni bendera ya Mungu, kwa kufanya jambo hilo: kwa kuweza kumwambia Filipo mahali alipokuwa; kumwambia mwanamke kuhusu kutokwa kwake na damu, na kadhalika; na—na mahali sarafu ilipokuwa, katika kinywa cha samaki; ama kitu kama hicho, kitu fulani; ya kwamba, yule mwanamke, ya kwamba alikuwa akiishi katika uzinzi, ama chochote kama hicho. Hilo hakika lilikuwa ni thibitisho Yeye alikuwa Masihi.

²⁰⁵ Sasa mwangalie yule Myahudi hodari, Filipo, wakati Filipo ama. . . Nathanaeli alipokuja. Nathanaeli alikuwa ni mwanazuoni, mwothodoksi halisi. Na wakati alipomwona Yesu, ilikuwa ni vigumu kwake kumwamini. Naye akasema, “Tazama Mwisraeli kwelikweli ambaye hamna hila ndani yake.”

Akasema, “Ulinijua lini, Bwana?”

Kasema, “Kabla Filipo hajakuita.”

Kasema, “Mwalimu, Wewe ni Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli.”

Yule mwanamke kisimani alisema, “Sina mume.”

Akasema, “Naam, una watano.”

²⁰⁶ Akasema, “Tunajua, Masihi atakapokuja, Yeye atatwambia mambo hayo. Lakini U nani Wewe?”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

“Tunajua ya kwamba hiyo itakuwa ndiyo bendera.”

²⁰⁷ Na kama Yesu Kristo ni bendera ile ile jana, leo, na hata milele, Yeye atafanya jambo lile lile kama anaweza kuushika moyo wa mwanadamu. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²⁰⁸ Sasa, mama huyu anayesimama hapa, simjui, sijapata kumwona. Hatufahamiani. Sivyo? [Huyo dada anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Hiyo ni kweli. Kama Mungu ataniambia shida yako ni nini, je! utaniamini? Unajua kama ni kweli ama si kweli, sivyo? [“Ndiyo.”] Je! ungekubali uponyaji wako basi? Uko mgongoni mwako. Umekwisha. Umeponywa. Hivyo ndivyo ilivyo. . . ? . . . Sasa nenda zako, na Mungu akubariki. Nenda.

²⁰⁹ [Huyo dada anasema, “Mwombee mwanangu.”—Mh.] Unaona? Mungu akubariki. [“Ndiye aliye na kansa katika ninii yake. . . ? . . .] Kama utaamini, moyo wako wote. Naam. Unaamini kwa moyo wako wote? Unaona? Kuwa tu na imani. Usitilie shaka. Amini.

²¹⁰ Sasa unaona jinsi lilivyo rahisi. Sasa, kama tukiomba tu. . . Sasa, unaona, Yeye anajua, kila mmoja wenu, ana shida gani. Mnaamini hilo, sivyo? Mnajua hiyo ni kweli. Sasa, kama nikimchukua tu mama huyu hapa, na kusema sitasema jambo lolote kulihusu, lakini niombe tu na kukuwekea mikono,

unaamini ungeponywa? Unaamini utaponywa? [Huyo dada anasema, “Ninaamini.”—Mh.] Vema. Inamisha kichwa chako, kwa dakika moja.

²¹¹ Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu. Jalia aondoke sasa. Tunaona bendera imeinuliwa. Tunajua ya kwamba Yeye atawavuta wote. Ninaweka mikono yangu juu ya dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

Usitilie shaka. Amini tu kwa moyo wako wote.

²¹² Ninasema, kama nisingesema jambo moja, nikuombe tu, ungali ungeamini jambo hilo. Sivyo? [Huyo dada anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Ungeamini, kwa vyovyote vile. Lakini kama nikikwambia, je! ingekusaidia? Ugonjwa wako wa moyo. Hiyo ni kweli. Nenda zako.

²¹³ Ingekusaidia kama ningekwambia shida uliyokuwa nayo? La, hu—hujui kama ingekusaidia ama haingekusaidia. Vema, labda nitakuombea tu.

²¹⁴ Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamsaidia mwanamke huyu. Mpe imani na nguvu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Amini sasa kwa moyo wako wote.

²¹⁵ Unafikiri nini, dada? Hatufahamiani. Kama Yesu angeniambia shida yako ni nini... [Huyo dada anasema, “Wewe si mgeni.”—Mh.] Ati si mgeni mimi? Ati unanijua, sasa? [“La. Nilikuona wakati ulipokuja mara ya kwanza.”] Uliniona nilipokuja mara ya kwanza. Hilo ni zuri. [“Mara ya kwanza.”] Ninamaanisha, sikujui wewe. [“Mara ya kwanza, haidhuru.”] Ati mara ya kwanza? [“Ndiyo. Uliniombea.”] Imekuwa karibu miaka kumi na mitano iliyopita. [“Ndiyo. Ni karibu kumi na mitano tu.”] Miaka kumi na mitano iliyopita. Jamani, imekuwa ni muda mrefu. [“Ndiyo, umekuwa ni muda mrefu.”] Ninii mengi—mambo mengi sana yametendeka tangu wakati huo. [“Ndiyo, yametendeka.”] Vema, itakubidi kufanyiwa upasuaji. [“Ndiyo.”] Bali kama utamwamini Kristo, uvimbe huo utakuacha, na haitakubidi kufanyiwa upasuaji. [“Amina.”] Unaamini jambo hilo? [“Ndiyo, bwana. Ninaamini.”] Basi nenda zako, amini jambo hilo.

²¹⁶ U hali gani? [Huyo dada anasema, “Umeniona hapo kabla.”—Mh.] Nimekuona. Lakini je! unaamini, kama nikimwomba Mungu, Yeye atakuponya? [“Ninaamini.”]

²¹⁷ Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya na kumpa afya, Baba. Ninaweka mikono juu yake, katika Jina la Yesu. Amina.

²¹⁸ Kama wewe... [Huyo dada anasema, “Ni neva zangu. Ni...?...”—Mh.] A-ha. Amini kwa moyo wako wote, nawe—wewe...?...Vema.

Njoo moja kwa moja, dada.

219 Sasa, mnaona, siwezi kuwaponya watu. Na Mungu hawezi kuponya watu isipokuwa watu waamini ya kwamba Kristo tayari amewaponya. Na sasa mnasema... Nilihubiri usiku wa leo juu ya kitu fulani ungaliweza kukishikilia kwa mikono yako. Yeye atasema, "Hiki hapa."

220 Sasa, mnaona, kama Yesu angelikuwa amesimama hapa Mwenyewe, amevaa suti hii aliyoweka moyoni mwa Ndugu Williams kunipa mimi...Lakini, Yeye, kama Yeye—kama Yeye angelikuwa amesimama hapa amevaa suti hii...Je! unajua, ninaamini ya kwamba yeye alimpa Bwana wakati alipofanya hivyo?

221 Ni wangapi waliopata kusoma maisha ya Mtakatifu Martin? Yeye alikuwa kafiri, pia alikuwa askari. Baba yake alitaka awe askari. Na yeye hakutaka kuwa askari. Yeye, kitu fulani kilimwita, kuhusu Mungu.

222 Ndipo usiku mmoja, alipokuwa akipitia mahali fulani, usiku wenye baridi sana wa majira ya baridi kali, kulikuwako na maskini mwombaji mmoja mzee, aliyekuwa amelala barabarani, akifa kwa kuganda kwa baridi. Na watu walipitia pale ambao wangeweza kumsaidia. Hawakumsaidia. Martin alikuwa ametoa kila kitu alichokuwa nacho. Kwa hiyo akasema, "Kuna jambo moja tu la kufanya. Nina koti moja." Kwa hiyo akautwaa tu upanga wake, akakata koti hilo nusu, vipande viwili, akamfunika mwombaji huyo nacho, namna hiyo, naye akaenda zake na hiyo nusu nyingine.

223 Watu walimcheka, wakisema, "Ni ujinga jinsi gani! Hivi yeye si ni askari mwenye sura nzuri sasa, akiwa amevaa nusu koti?" Hakuwajali kamwe, akaendelea mbele, maana alijua ndivyo alivyopaswa kufanya.

224 Usiku huo katika kambi za jeshi, yeye aliamka. Na alipoamka, alimwona Yesu amesimama pale, amevikwa kile kipande cha koti alichokuwa amemfunika yule mwombaji nacho.

225 Naye akawaangalia Malaika. Akasema, "Je! mnajua ni nani aliyenivika hiki?"

Wakasema, "La."

Akasema, "Nilivikwa na Martin."

226 Haya basi. Yeye alifanyika mtakatifu, akinena kwa lugha, na kutoa pepo, akiona maono, nabii mwenye nguvu wa Mungu. Naam, bwana. Kwa nini? Wakati alipomvika maskini mwombaji huyo mzee hapo barabarani, alimvika Yesu Kristo. "Kadiri mlivyomtendea aliye mdogo sana wa hawa watoto Wangu, mmenitendea Mimi."

227 Na kuwa na uhakika ya kwamba mmevikwa haki ya Kristo, ninajaribu kuwaambia usiku wa leo. Kama ningalikuwa

na nguvu za kuwaponya, ningalimponya kila mmoja wenu. Mnaona? Lakini ninajaribu kuwaonyesha kwa karama, kuhusu yale niliyohubiri, ya kwamba Mungu anayathibitisha kuwa ni kweli, unaona, ya kwamba siwezi kuwaponya watu, bali ni kuwafanya mjue ya kwamba Yeye yupo hapa.

228 Unaamini hilo, mama? Basi Yabisi kavu yako itakuacha. Unaamini itakuacha? Basi nenda zako na kupaza sauti, na kusema, “Bwana asifiwe. Ninaamini kwa moyo wangu wote.”

229 Hilo nililosema lilikuwa ni jambo la kuchekesha, ambalo nilisema, “yabisi kavu,” kwake, nawe ulikuwa na kitu kile kile. Endelea tu uende, useme, “Ninaami kwa moyo wangu wote,” na uende tu. Itatendeka.

230 Sasa je! unaamini ya kwamba Mungu ataponya tumbo lako, nawe uende nyumbani na ule kama vile unavyopaswa kula? [Huyo dada anasema, “Bwana asifiwe.”—Mh.] Basi nenda zako nyumbani moja kwa moja na ule kama vile unavyopaswa kula.

231 Amini sasa. Unaamini kwa moyo wako wote? “Kama ni—kama nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta watu wote Kwangu.”

232 Sasa, je! unaamini ya kwamba Roho Mtakatifu yupo hapa? Kama nikikuwekea tu mikono, u—ungeponywa? [Huyo dada anasema, “Hakika ninaamini.”—Mh.]

Katika Jina la Yesu, na aponywe.

233 “Ishara hizi zitafuatana na hao wanaoamini katika Jina Langu.” Sasa, aminini sasa tu mnapopitia hapa.

Njoo moja kwa moja, dada.

Katika Jina la Yesu Kristo!

234 Kila mtu aombe sasa. Unaona, wingi wa maono hayo hunidhoofisha, unaona. Unaona?

Katika Jina la Yesu, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu.

235 Nilikuona ukiinua mkono wako pale, ya kwamba unaamini. [Huyo dada anasema, “Ninaamini.”—Mh.] Amini sasa. [“Ndiyo.”]

Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba ya kwamba utamponya.

Njoo, dada.

236 Baba, Mungu, sina cha mkononi nikuleteacho. Nashikilia tu msalaba Wako. Ninaomba kwa ajili ya uponyaji wake, katika Jina la Yesu. Amina.

237 Baba, Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, jalia dada yetu aponywe. Amina.

Njoo, ndugu yangu mpendwa.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia ndugu yangu aponywe.

238 Unaamini ya kwamba Mungu atamponya na kumpa afya? [Huyo dada anasema, “Hakika ninaamini.”—Mh.]

Katika Jina la Yesu Kristo, mtoto huyu na aponywe.

Sasa angalia tu, kwa kuwa ameombewa sasa.

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yetu na aponywe.

Katika Jina la Bwana Yesu, dada yetu na aponywe.

Katika Jina la Bwana Yesu, dada yetu na aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yetu na aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yangu na aponywe.

Sasa, endeleeni kuomba, kila mtu, kimya kabisa, katika maombi.

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yetu na aponywe.

Ee Mungu, mrudishie msichana huyu mdogo kile kilichochukuliwa na Shetani.

Ondoka ndani yake, Shetani! . . . ? . . .

Katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yetu na aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yetu na aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yetu na aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yetu na aponywe.

Katika Jina la Bwana Yesu, dada yetu na . . . ? . . .

Katika Jina la Bwana Yesu, dada yetu na . . . ? . . .

Katika Jina la Yesu Kristo, nanii wetu . . . ? . . .

239 Sasa, katika wasikilizaji, kila mmoja. Ninajua mtu fulani hakupata kadi za maombi za kutosha huko. Ninataka uinamishe kichwa chako, kwa dakika moja. Ninataka kukuuliza swali.

240 Miaka elfu mbili iliyopita kulikuwako na Mtu. Miaka elfu nne, naam, yapata miaka elfu mbili mia tano iliyopita, kulikuwako na ninii. . . Mungu alishuka, akiwakilishwa katika Mwanadamu, naye akaketi kwenye mwa—mwaloni wa Ibrahimu. Akaelekeza mgongo Wake kwenye ukuta, samahani kwenye hema, akamwambia Sara shida ilikuwa ni nini, akiwa ndani. Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku ile, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.”

241 Yesu alikuwa bendera ya Mungu. “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Tunaona jambo hilo. Ni kweli, bila shaka.

242 Sasa, sababu ya mimi kutoendelea mbele, nina mikutano mingi sana. Nitarudi Phoenix siku moja, nikiwa na mkutano mkuu, Bwana akipenda.

243 Sasa, kwenu ninyi hapa usiku wa leo mlio wagonjwa na wahitaji, na hamkupata kadi ya maombi, kuja madhabahuni,

hapa juu kuombewa, nitawaombea sasa. Ninawatakeni mwe na kicho sana.

²⁴⁴ Ninataka kila mmoja wenu ninyi waaminio mwekeane mikono, kama—kama ishara. Sasa, Biblia ilisema, sasa, Mungu yuyu huyu aliyefanya ahadi hii, alisema hivi, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Mwaminio yeyote, mwaminio yeyote aliye na Roho Mtakatifu, una nguvu za Mungu ndani yako, ama mamlaka, kuomba ombi la imani. Ninataka uombe wakati nikiwaombea watu hawa.

²⁴⁵ Baba yetu wa Mbinguni, tuna furaha usiku wa leo. Kulihubiri Neno, kisha kuona Mungu akishuka chini na kuthibitisha hilo Neno, basi hiyo—hiyo ndiyo bendera uliyohidi.

²⁴⁶ Siku moja, zamani za kale, kulikuwa na mvulana mdogo jina lake Daudi. Alikuwa akichunga kondoo wa baba yake. Alipewa jukumu la kuwachunga kondoo hawa, kuwakinga na adui. Alikuwa na vitu vichache sana vya kujikinga navyo, kombeo dogo tu. Lakini siku moja simba aliingia kambini, naye akamchukua mmoja wa hao wana-kondoo. Daudi, akiwa ni mchungaji wa kweli, alitaka kumshikilia mwana-kondoo huyo wa baba. Alijua ya kwamba huyo simba alikuwa akimwiba kondoo huyo, naye angemla kondoo huyo, na huyo kondoo alikuwa ni mali ya baba yake. Alimwendea huyo simba akiwa na ushujaa hodari. Alirusha jiwe dogo, nalo likamwangusha huyo simba chini. Naye akamwua huyo simba, na kumrudisha kondoo zizini.

²⁴⁷ Sasa, Mungu, sisi ni wachungaji Wako wa kondoo. Sisi si watu wa kufanya upasuaji kwa visu ama wa—wa kuponya kwa dawa. Tuna kitu kidogo sana na rahisi, kombeo. Lakini hilo ndilo umeweka mkononi mwetu, kombeo la maombi. Adui ameingia na kunnyakua kondoo wa Mungu. Amewanyakua akina baba, na akina mama, na watoto, akiwaburuzia vichakani sasa; akili taahira, na vipofu, na walioliwa na kansa, na pepo.

²⁴⁸ Shetani, kombeo hili dogo la maombi linaonekana rahisi sana, bali ninajua kile litakachofanya. Ninamfuatia kondoo huyo usiku wa leo, kumrudisha. Toka. Mwache. Toka ndani ya mtu huyo, ewe pepo mchafu wa magonjwa, na umwache. Ninakuapiza, katika Jina la Yesu Kristo, ondoka, wala usiwarudie tena. Mungu wa Mbinguni na akukemee, ewe Shetani.

²⁴⁹ Yesu wa Nazareti alisema, “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usitilie shaka moyoni mwako, bali uamini uliyosema, yatakuwa yako.” Kwa hiyo, katika Jina la Yesu Kristo, ninatamka ukombozi kwa kila mtu hapa. Kwa ninii. . .

²⁵⁰ Shetani, huenda ukasema hatuna mamlaka ya kufanya jambo hili. Tunakuonyesha bendera usiku wa leo, Yesu Kristo.

Roho Mtakatifu yupo hapa, akithibitisha ya kwamba hii ndiyo bendera ya Mungu, nawe umeshindwa vita. Toka, katika Jina la Yesu Kristo.



BENDERA SWA62-0119

(An Ensign)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, tarehe 19 Januari, 1962, katika Kanisa la Jesus Name huko Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2013 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org